Nipashe

Ijumaa Januari 17, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581924 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 Nipashe Digital

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

UKURASA WA 2

**Wenje** amjia juu Lema akimtuhumu kuhusika njama za kumpindua Mbowe

UKURASA WA 4

**Mume** na mke watumbukizwa chooni, majambazi waondoka na gari, kichanga chao

UKURASA WA 5

**NIDA** kusitisha matumizi namba ya utambulisho wasiochukua kadi zao



**NEYMAR AWINDWA NA TIMU TATU MAREKANI** UK. 21




Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu akizungumza na wahariri na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu nia yake ya kugombea Urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Dorothy Semu ajitosa urais akiwa na hoja nne

UKURASA 3

# 204 watumia mafuta ya kupikia, wadhurika

• **Mwuzaji** wa jumla atiwa mbaroni, DC aunda timu, TBS yachunguza... *Ukurasa 2*



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete na mkewe, Mama Salma Kikwete akiwa katika kituo cha treni ya reli ya kisasa (SGR), jijini Dar es Salaam jana, tayari kuelekea katika Jiji la Dodoma, kushiriki mkutano mkuu maalumu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa utakaofanyika kesho na kesho kutwa. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## JK aambatana katika SGR na wajumbe 700 Mkutano Mkuu CCM Dodoma

UKURASA 18

**MICHEZO** **YANGA INA NJAA YA USHINDI** UK.24

**MAONI,** UK.6



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# 204 watumia mafuta ya kupikia, wadhurika

**Na Restuta James**

TAKRIBANI wakazi 204 wa Mtaa wa Yombo Dovya, Temeke mkoani Dar es Salaam, wameathirika kwa kubabuka ngozi katika maeneo mbalimbali ya mwili, baada ya kudaiwa kutumia mafuta ya kula yenye sumu.

Wakazi hao wanaonekana kubabuka ngozi na kuota malengelenge sehemu mbalimbali za mwili, maumivu makali ya kichwa, kutapika na kuharisha.

Wakizungumza jana Dar es Salaam, baadhi ya wakazi hao walisema wameathiriwa na mafuta na kwamba walianza kupata maumivu makali muda mfupi baada ya kula chakula kilichopikwa kwa mafuta hayo.

Mkazi wa Yombo Dovya, anayefanya biashara ya chapati, ambaye hakutaja jina lake, alisema alinunua mafuta ya kupikia dukani ambayo aliyatumia kukaanga chapati kama kawaida ambazo hata yeye alikula.

"Nilipomaliza kufanya biashara, nikachukua chapati mbili nikala.Ilipofika saa9:00 alasiri, nikaona mabadiliko makubwa sana kwenye mwili wangu. Kikaanza kichwa, shingo haipinduki na mdomoni vidonda tayari vikawa vimetoka," alisema.

Mkazi mwingine, alisema alinunua chapati kwa mama huyo na muda mfupi baada ya kula, alianza kupata maumivu makali ya kichwa hali iliyomlazimu kulala.

"Hali ilivyokuwa mbaya nikaenda kununua maziwa, nikanywa. Baada ya kunywa tu nikaanza kutapika nikahisi kabisa kwamba hii itakuwa sumu," alisema.

Mkazi mwingine, alisema mafuta hayo yamewaathiri zaidi watoto ambao wametapika na kuharisha pamoja na kubabuka ngozi, maumivu makali ya kichwa na kupata vidonda kama malengelenge.

Muuzaji wa mafuta hayo aliyetajwa kwa jina moja la Kamau maarufu kama Mangi, alisema alipokea malalamiko ya wateja kuumwa baada ya kutumia mafuta anayouza, jambo lililomlazimu kuyabadili na kuuza dumu lingine, lakini hali ya wateja haikubadilika.

"Mafuta niliagiza kama madumu 20 hivi, nikawa nauza kama kawaida. Nikapokea changamoto kutoka kwa wateja na sikupuuza. Nikayarudisha kwenye dumu, nikafungua dumu jipya, lakini malalamiko hayakuisha," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Dovya, Denis Moyo, alisema alipokea taarifa za maumivu yaliyosababishwa na mafuta ya kula, ndipo alipochukua hatua ya kuwapeleka Kituo cha Afya, kwa uchunguzi.

"Tumeingia kila nyumba, Kitongoji chote hiki, tumebaini jumla ya watu 204 wenye dalili za moja kwa moja za matatizo haya. Tukiwauliza, mwingine anasema alikula chapati, mwingine kitumbua, maandazi, chakula au chipsi," alisema Moyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda, alisema tayari ameunda timu kuchunguza mafuta hayo na kwamba muuzaji wa jumla aliyetajwa kwa jina la Ali Hafidh 'Mpemba', amekamatwa.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini kwamba madumu ya mafuta hayo, hayana 'seal'.

"Tulikuta madumu 99 hayana seal, alipoulizwa sababu za madumu hayo kutofungwa vizuri alisema wanapoyanunua jumla wanaondoa seal ili wasafirishe vizuri," alisema Mapunda.

Alisema maelezo hayo yameongeza mashaka na kwamba madumu hayo yamezuiwa ili kufanyiwa uchunguzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na muuzaji huyo anashikiliwa na vyombo vya dola.

Alisema wananchi walioathirika wameshatibiwa na kuruhusiwa na kwamba kinachosubiriwa hivi sasa ni taarifa ya TBS ili kubaini kiini cha tatizo la mafuta hayo.

"Wananchi wametibiwa na wote wamesharuhusiwa kurudi nyumbani," alisema.


PUBLIC NOTICE



*Mr. Humphrey Joshua Kajela*

118328702

We would like to inform our stakeholders and the General public that **Mr. Humphrey Joshua Kajela** is no longer employed with **LOLC Tanzania (Previously Tujijenge Tanzania Financial Service Limited)**

For official communication with Tujijenge Tanzania Financial Services please contact **+255 739 611 611/+255 739 611 612**


# Wenje amjia juu Lema akimtuhumu kuhusika njama kumpindua Mbowe

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Kanda ya Victoria wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ezekia Wenje amemjia juu Godbless Lema, akidai ni miongoni mwa makada waliosuka mpango wa kumpindua Mwenyekiti wao, Freeman Mbowe alipokuwa gerezani.

Amedai kuna baadhi ya wanachama wa chama hicho, wakiongozwa na Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini, Lema, walianzisha mpango uliopewa jina la 'Join the Chain'.

Alisema mpango huo ulikuwa na dhumuni la kukusanya fedha za kuwezesha kuitishwa kikao cha Baraza Kuu na Kamati Kuu ya chama hicho kuwashawishi wajumbe kufanya mapinduzi ya kumteua Tundu Lissu kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na Mch. Peter Msigwa awe Makamu Mwenyekiti wake.

Wenje alidai hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari, akisema: "Mnakumbuka mimi, Lema na Lissu tulikimbia nchi, tukiwa huko mafichoni huku nyumbani mambo yakatokea mengi mpaka Mwenyekiti (Mbowe), akakamatwa akafungwa gerezani.

"Mwaka 2022, (Mbowe) akiwa gerezani, marafiki zangu hawa wakashauriana kwamba waanzishe kitu kinaitwa 'Join the Chain' na Mwenyekiti aliyeasisi hiyo 'movement' ni rafiki yangu, Godbless Lema."

Alidai viongozi hao waliamini kuwa Mbowe kukabiliwa na kesi ya ugaidi asingetoka mahabusu gerezani kwa urahisi.

Wenje alidai kuwa baada ya kushirikishwa mpango huo, aliamua kujiweka pembeni, akisisitiza uamuzi wake huo ukawa mwanzo wa matatizo na tofauti za kimtazamo kati yake na viongozi hao waliokuwa wakipanga njama.

"Niliposhirikishwa mambo kama haya, nilikataa uasi na hii ndiyo sababu kubwa ya kuanza kwa ugomvi mkubwa kati yangu na marafiki zangu, mimi nilikataa kuwa mwasi, nikajiondoa kwenye process (mchakato) yote," alidai Wenje.

**ZITTO KUFUKUZWA**

Kadhalika, Wenje alidai kuwa hata mpango wa kumfukuza uanachama Zitto Kabwe (wakati huo akiwa CHADEMA), uliongozwa na Lema.

"Hivi ninavyovieleza, hata Mbowe anavijua. Kama si uvumilivu, watu wanaopanga kufanya mapinduzi ndani ya chama bila kufuata Katiba, kina Lema, ndiyo watu ambao hawakupaswa kuwa wana-CHADEMA," alidai Wenje ikiwa ni majibu kwa Lema ambaye juzi alisisitiza kuwa kama angekuwa na mamlaka kichama, Wenje asingekuwa mwanachama wao.

Kuhusu yeye kudaiwa kutumwa na Mbowe kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA kwa madai ya kumwondoa Lissu, Wenje alidai "hayo ni mawazo ya kidikteta" ya kutopenda agombee.

LEMA KUSUSA

Kadhalika, Wenje alidai anamshangaa Lema kumtishia Mbowe kuwa akishinda tena nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, hatogombea ubunge wa Arusha Mjini.

"Yeye kama hana ushawishi huko Arusha, anaona mambo ni magumu, aseme tu! Hivyo vingine ni visingizio vidogo vidogo. Ukweli ni kwamba Lema angegombea uenyekiti wa chama Kanda ya Kaskazini angeshindwa vibaya sana, alisoma upepo. Kwa hiyo alikula kona mapema," alidai Wenje.

Mwanasiasa huyo pia alisema yeye na wenzake wako upande wa chama na si upande wa Mbowe kama inavyodaiwa.

Wenje alidai kwamba kuna taarifa amezipata kwamba Lema na wanachama wengine wanapanga kuhama chama hicho endapo watashindwa kwenye uchaguzi huo.

Kadhalika, Wenje alimshutumu Lissu kukimbia kuongoza chama hicho wakati Mbowe akiwa gerezani na kwamba alitegemewa awe miongoni mwa mawakili wa kuongoza jopo la utetezi wakati Mbowe yuko gerezani.

Wenje pia alidai kuwa mpaka sasa Mbowe ndiye mgombea anayeungwa mkono zaidi kuliko ilivyo kwa Lissu.

Katika hilo, Wenje alidai kuwa katika kanda tisa ambazo zimefanya uchaguzi wa ndani wa chama mpaka sasa, viongozi wa kanda nane wanamuunga mkono Mbowe.

Pia alidai wenyeviti na makatibu wengi wa mikoa wa chama hicho wanamuunga mkono Mbowe na ndiyo waliokwenda nyumbani kwake kumshawishi agombee tena kuongoza chama hicho.

Uchaguzi wa viongozi wakuu wa CHADEMA umepangwa kufanyika siku nne zijazo katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

HABARI KITAIFA

## DOROTHY SEMU
# Ajitosa urais akiwa na hoja nne

**Na Mwandishi Wetu**



KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu (pichani) ametangaza rasmi nia ya kugombea nafasi ya Rais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Amesema kusudio lake hilo limesukumwa na mambo manne anayoona yamekuwa kero kubwa nchini katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita.

Akitangaza kusudio lake hilo jana alipozungumza na wahariri na waandishi wa habari kwenye ofisi ya Makao ya Makuu ya chama hicho iliyoko Magomeni, Dar es Salaam, Dorothy alitaja mambo yaliyomsukuma ni pamoja na kushuka kwa kasi ya ukuaji uchumi.

Katika hilo, Dorothy (50) alisema kuwa licha ya serikali kueleza kwamba uchumi unakua, Ripoti ya Benki ya Dunia (WB) ya Mwaka 2024 inaonesha kuwa kasi ya ukuaji uchumi nchini imeshuka kutoka asilimia 6.8 mwaka 2019 hadi asilimia 4.6 mwaka 2023.

"Kupungua huku kumetokana na sera zisizo thabiti za uwekezaji na utekelezaji hafifu wa miradi ya maendeleo," Dorothy alisema.

Alitaja jambo la pili ni kupanda kwa gharama za maisha, akifafanua kuwa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonesha kiwango cha mfumuko wa bei kilifikia asilimia 5.6 mwaka 2023 kulinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2020.

Katika hilo, Dorothy alisema hali hiyo imeendelea kuwa inajirudia na inaathiri uwezo wa wananchi kumudu mahitaji ya msingi, hususani vyakula na huduma za afya.

Dorothy alitaja jambo la tatu ni changamoto za ajira kwa vijana, akiwa na ufafanuzi kuwa Ripoti ya Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini Tanzania (REPOA) ya Mwaka 2019, inabainisha kuwa takribani vijana milioni moja wanahitimu vyuo kila mwaka huku wanaoajiriwa serikalini na sekta binafsi ni 250,000 tu.

"Kwa wastani wa kila mhitimu anatumia wastani miaka 5.5 kupata ajira. Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan na CCM yake imeshindwa kuwekeza vya kutosha katika sekta zinazoweza kuzalisha ajira kama kilimo, viwanda, na teknolojia," alisema.

Dorothy alitaja hoja ya nne ni udhaifu katika usimamizi wa rasilimali za taifa, akieleza kuwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Mwaka 2023 inabainisha upotevu wa Sh. bilioni 450 kupitia miradi iliyosimamiwa vibaya na mikataba isiyo na uwazi.

"Hali hii ni ishara ya kushindwa kudhibiti ufisadi na matumizi mabaya ya rasilimali za umma. Ndugu zangu, Tanzania inahitaji uongozi mpya utakaolinda maslahi ya taifa na uchumi imara, jamii yenye fursa sawa na uongozi wa uwazi.

"Tunaweza kubadilisha hali hii kwa kushirikiana, kuondoa changamoto hizi na kuimarisha mustakabali wa taifa letu. Niko tayari kumkabili Samia Suluhu Hassan kwenye uchaguzi wa 2025 endapo chama changu cha ACT Wazalendo kitanipa ridhaa," Dorothy alihitimisha kutangaza nia yake hiyo katika hotuba iliyochukua dakika tano tu.

Akitangaza msimamo wa ACT Wazalendo kuhusu kushirikiana na vyama vingine vya upinzani mwaka huu baada ya kuulizwa na waandishi wa habari, Dorothy alisema wako tayari kufanya hivyo ikiwa kutafanyika mazungumzo ya kukubaliana kuachiana baadhi ya maeneo kama ilivyofanyika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

"Tuko tayari kushirikiana na vyama vingine vya upinzani, hata kuachiana katika baadhi ya maeneo ikibidi. Lakini hilo litahitaji kufanya majadiliano. Sote ni mashahidi kwa kilichovunwa na upinzani mwaka 2015.

"Upinzani tulipata kura za urais kwa asilimia 44 na tukawa na idadi kubwa ya wabunge na madiwani. Hivyo, watanzania tunapaswa kukumbatia utaratibu huu," alisema.

**KUHUSU DOROTHY**

Dorothy alizaliwa mwaka 1975 na wazazi waliokuwa watumishi wa umma na kukulia jijini Arusha na mkoani Kilimanjaro.

Ana Shahada ya Uzamili katika Tiba ya Mwili (Physiotherapy) kutoka Chuo Kikuu cha Western Cape, Afrika Kusini, akitumikia serikalini kwa miaka 17.

Kazi zake zilihusisha kutibu wagonjwa na kusimamia programu za afya, hasa katika eneo la kudhibiti ulemavu utokanao na ukoma.

Uzoefu wake wa kazi ulimwezesha kuboresha takwimu za kitaifa kuhusu huduma za afya kwa watu walioathiriwa na ukoma.

Dorothy aliamua kuchukua hatua zaidi katika kupigania usawa na kuboresha maisha ya watanzania kwa kuingia katika siasa, akijiunga na chama cha ACT Wazalendo na kufanya kazi kama Katibu wa Sera na Utafiti wa chama hicho.

Alifanya kazi kama Katibu Mkuu wa ACT- Wazalendo kati ya mwaka 2017 na 2020 kisha kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Bara. Alikuwa Waziri Mkuu Kivuli wa ACT Wazalendo kuanzia mwaka 2020 mpaka mwaka 2022.

Machi 6, 2024 alichaguliwa kuwa Kiongozi wa ACT Wazalendo, akichukua nafasi ya Zitto Kabwe aliyemaliza muda wake.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***





Mkazi wa Galagaza, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Melkisedeck Mrema akionesha sehemu alipotumbukizwa mke wake na watekaji walioondoka na mtoto wake wa miezi saba pamoja na gari. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

# Mume, mke watumbukizwa chooni, majambazi waondoka na gari, mtoto wa miezi saba

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

MKAZI wa Galagaza, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Melkisedeck Mrema amenusurika kufa baada ya kutumbukizwa kwenye shimo la choo na watu waliovamia nyumbani kwake na kumteka mtoto na mke wake.

Saa 10 baada ya tukio hilo, mke wake, Johari Bung'ombe alipatikana akiwa katika shimo la choo nyumba ya jirani alipotumbukizwa na watu hao mita chache kutoka nyumbani kwake.

Akisimulia tukio hilo, Mrema alisema Januari 15 majira ya saa 12 asubuhi alitoka nje ya nyumba yake ili kuhudumia kuku, ghafla walitokea watu hao kwa nyuma na kumpiga kichwani.

Alipogeuka aliwaona wakiwa na nondo, panga na kisu na kuamua kupiga kelele kuomba msaada, lakini walimpiga tena na panga wakimtaka kukaa kimya huku wakimsukuma kurudi ndani.

Alisema walimwingiza ndani na kufunga milango kwa funguo na kumtaka atoe fedha alizo nazo jambo ambalo alipingana nao na kuendelea na purukushani na watu hao.

"Wakiwa wameniweka chini ya ulinzi sebuleni kwangu, mke na mwanangu walikuwa chumbani, walivunja mlango na kuwaleta nilipo," alisema.

"Walipoingia chumbani walimshurutisha mke wangu akawapa fedha iliyopo wakanirudia tena kunipiga nionyeshe nilipoweka hela, nilimwambia iliyopo ndio waliyoichukua, lakini hawakunielewa waliendelea kunishurutisha," alisema.

Mrema alisema mbali ya fedha walichukua simu zote zikiwamo anazotolea huduma ya fedha na kumtaka awape nywila (password), ili waangalie miamala wakatoe fedha zilizopo.

"Niliwapa ili niokoe maisha yangu, mwanangu na mke wangu ambaye ni mjamzito. Hata hivyo, haikusaidia walinifunga mikono na miguu wakanitoa nje huku mke na mwanangu wakiwarudisha chumbani."

Mrema alisema walipotokea nje walimpeleka kwenye karo la shimo la choo wakawa wanalazimisha kumwingiza ndani, lakini kutokana na kumfunga mikono ilishindikana.

"Niliwaambia wanifungue mikono ili waniingize, walifanya hivyo na kunisukuma ndani kwa miguu nikadondokea shimoni, wakafunga na kuondoka sikujua walielekea wapi," alisema.

Akiwa ndani ya shimo, Mrema alisema alipata mti ambao aliutumia kugonga juu ya mfuniko huku akipiga kelele kuomba msaada, hata hivyo alitokea mmoja wa wateja wake ambaye alimkosa kwenye simu na kumfuata nyumbani ndipo aliposikia sauti yake na kufunua shimo.

"Kuna mtu nilikua na ahadi naye aliponikosa kwenye simu na dukani sijafungua alikuja nyumbani majira ya saa mbili hivi, aliposikia nagonga kwenye shimo alifunua nikamuomba anisaidie nitoke. Alitoa taarifa kwa mwenyekiti na majirani wakaja na kamba kunitoa," alisema.

Alisema wakati anatolewa kwenye shimo, alitarajia kumkuta mke wake na mtoto wao wa miezi saba wakiwa ndani, lakini alikuta nyumba imefungwa kwa ufunguo na hakukuwa na mtu ndani.

Mrema aliendelea kusimulia kuwa baada ya kumaliza taratibu za kutoa taarifa za polisi na hospitali, walirudi nyumbani na aliwashauri kuzunguka maeneo ya vichaka na nyumba za jirani kuwaangalia mama na mwanawe.

Mita chache kutoka nyumbani kwake alipita kwenye shimo la choo na kusikia sauti ikiomba msaada, alipojaribu kufunua ikashindikana kutokana na mikono yake kukosa nguvu ndipo alipoomba msaada kwa watu waliokuwa karibu na eneo hilo.

"Walikuja wakafunua tulimkuta mke wangu ndani amechoka baada ya kukaa kwa muda mrefu, nje ya shimo pembeni ya ufuniko hawa watekaji waliziba na majani ionekane kama yameota muda mrefu," alisema.

Mrema alisema mke wake ambaye yupo hospitali kwa matibabu alimweleza kwamba watekaji hao baada ya kumwingiza kwenye shimo hilo walisikika wakisema mtoto inabidi wakamchukue asibaki ndani peke yake.

Hadi saa kumi jioni Januari 16, Nipashe ilipotoka nyumbani kwa Mrema hakukuwa na taarifa ya kupatikana kwa mtoto wala gari.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Galagaza, Said Siasa, alisema wanaendelea kutoa ushirikiano kwa familia hiyo kumsaka mtoto pamoja na wahalifu hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Salim Morcase, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwa operesheni ya kuwasaka watu hao inaendelea.

Kamanda Morcase alisema mafanikio ya awali yaliyopatikana ni kumpata mke wa Mrema Januari 15 majira ya saa 11 jioni na uchunguzi wa tukio hilo unaendelea.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Laini za simu 12,896 zinazotumika kutapeli zafungwa

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imefunga laini za simu 12,896 kutokana na kujihusisha na vitendo vya ulaghai wa mtandaoni kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Ripoti ya utendaji wa TCRA iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. Jabiri Bakari ilibainisha kupungua kwa asilimia 19 ya matukio ya ulaghai kwa njia ya simu nchini.

Alisema idadi ya laini za simu zinazotumika katika masuala ya udanganyifu zimepungua kutoka 16,002 Julai na Septemba 2024 hadi 12,896 kipindi cha Oktoba na Desemba 2024, ikiwa ni punguzo la laini 3,106.

"Mikoa iliyoathiriwa zaidi na utapeli wa simu kwa kipindi hicho ni Rukwa (matukio 5,305), Morogoro (4,278), Mbeya (930), Dar es Salaam (765), Katavi (281), Arusha (260), Songwe (150), Mwanza (132) na Tabora (122).

"Ripoti hii pia inaonesha kuongezeka kwa majaribio ya udanganyifu kwenye mitandao na asilimia kwenye mabano, Halotel (sita), TTCL (12) na Airtel (52). Hata hivyo, majaribio ya udanganyifu kwenye mitandao ya Yas na Vodacom yalipungua kwa asiliamia 75," alisema Dk. Jabir akinukuu ripoti hiyo.

Aliongeza kuwa baadhi ya maeneo, hususani Zanzibar, yaliripotiwa matukio machache ya udanganyifu ikiwamo Kaskazini Pemba tukio moja, Kusini Pemba mawili, Mjini Magharibi moja, Kaskazini Unguja matano na Kusini Unguja matano.

Kadhalika, Dk. Bakari alisisitiza umuhimu wa matumizi salama na ya kuwajibika ya mifumo ya simu kwa ukuaji endelevu wa nchi na uboreshaji hali ya maisha ya wananchi.

Aliwahakikishia wananchi kwamba TCRA itaendelea kufuatilia na kubaini simu za udanganyifu zinazoingia nchini, kuchukua hatua stahiki ambazo zimesababisha kupungua kwa matukio yanayoripotiwa.

"TCRA imekuwa inasimamia uzuiaji simu zilizoibwa, kupotea au kuharibika zisitumike, pamoja na simu zisizokidhi viwango vinavyostahili au ni ghushi. Juhudi zetu pia ni pamoja na kutambua na kuzima nakala za IMEI namba zinazohusishwa na shughuli za ulaghai," alisema.

Alisema TCRA inaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi salama ya simu za mkononi ili kuwalinda watumiaji dhidi ya matapeli wa mtandaoni.

Vilevile, alisisitiza umuhimu wa wananchi kuwa waangalifu na kuwahimiza kuripoti ujumbe au simu zinazotiliwa shaka, Pamoja na kuwashauri kutuma namba za simu zinazohusishwa na matapeli kwenda 15040 kwa njia ya SMS.

Alisema huduma hiyo ni bure na kwamba hatua za udhibiti ikiwa ni pamoja na vikwazo zitatekelezwa kulingana na ripoti hizo.

# NIDA kusitisha matumizi namba ya utambulisho wasiochukua kadi zao

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imewataka wale wote ambao hawakujitokeza kuchukua vitambulisho vyao vya taifa vilivyopelekwa ofisi za kata, vijiji, mitaa, vitongoji na shehia kufika kwenye ofisi za NIDA za wilaya walikojisajili kuchukua vitambulisho vyao mara watakapopokea ujumbe mfupi wa maandishi katika simu zao za mkononi unaowataka kufanya hivyo.

Pia imetoa angalizo kuwa atakayeshindwa kufanya hivyo, matumizi ya Namba ya Utambulisho wake wa Taifa (NIN) yatasitishwa baada ya mwezi mmoja tangu kupokea ujumbe huo.

Hatua hiyo imechukuliwa ili kuhakikisha vitambulisho vyote vilivyozalishwa na kupelekwa katika ofisi za kata, vijiji, mitaa, vitongoji na shehia ili wananchi wavichukue huko, vinachukuliwa na wahusika.

Awali NIDA baada ya mwezi Oktoba 2023 mpaka Machi 2025 kuendesha zoezi maalumu la kuzalisha vitambulisho kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya wananchi wengi waliokuwa na NIN pekee kwa muda mrefu, ilivipeleka vitambulisho hivyo kwenye ofisi za kata, vijiji, mitaa, vitongoji na shehia ili kuondoa usumbufu kwa wananchi kuchukua vitambulisho hivyo badala ya kuvifuata katika ofisi za NIDA za wilaya.

"Tulipeleka vitambulisho vingi sana chini kwa wananchi katika ofisi za vijiji na mitaa yao ili kuwarahishia wananchi kupata vitambulisho hivyo, lakini kuna vitambulisho havijachukuliwa na wahusika, hivyo tumevikusanya vyote na kuvirejesha katika ofisi za NIDA za wilaya," alisema Geofrey Tengeneza, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha NIDA.

> **"Tulipeleka vitambulisho vingi sana chini kwa wananchi katika ofisi za vijiji na mitaa yao ili kuwarahishia wananchi kupata vitambulisho hivyo, lakini kuna vitambulisho..."**

Tengeneza alisema jana kuwa mamlaka imekamilisha ukusanyaji vitambulisho vyote kutoka ofisi hizo za kata, vijiji na mitaa na kuvirejesha katika ofisi za NIDA katika wilaya zote nchini na tayari ujumbe mfupi wa simu za mkononi (SMS) umeanza kutumwa na wananchi wameanza kujitokeza kuchukua vitambulisho vyao.

Aliongeza kuwa hatua hiyo ni utekelezaji maelekezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Innocent Bashungwa aliyotoa kwa mamlaka hiyo kuhakikisha vitambulisho vyote ambavyo havijachukuliwa va wahusika, vinachukuliwa ndani ya miezi miwili.

Itakumbukwa kuwa NIDA ilitengeneza vitambulisho vya taifa vingi kuanzia Septemba 2023. Oktoba 12, 2023 ilizindua ugawaji mkubwa wa vitambulisho hivyo kwa wananchi kwa kuvisambamba katika ofisi za kata, vijiji, mitaa na shehia kote nchini, zoezi lililokamilika Machi 2024.

Licha ya hatua hiyo ya NIDA, kuna wananchi zaidi ya milioni moja hawajachukua vitambulisho vyao, hali iliyosababisha vitambulisho vyao kuendelea kubaki katika ofisi hizo kwa muda mrefu.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# TCCA kuongeza safari za ndege, kulinda anga

**Na Moshi Lusonzo**

MAMLAKA ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imesema inatekeleza mkakati wa kuongeza safari za ndege nchini kwa kuhakikisha anga la Tanzania linaendelea kuwa salama na kuwa kivutio kwa mashirika ya ndege ya kimataifa.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Salim Msangi, alisema serikali kupitia mamlaka hiyo inaendelea kuboresha miundombinu na kusimamia sheria na kanuni ili watu wengi kutumia usafiri wa ndege kupitia katika viwanja mbalimbali nchini.

Msangi alisema wanaendelea kufanya maandalizi kwa ajili ya ukaguzi wa Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) na kwa sasa TCAA inahuisha kanuni za usafiri ili ziendane mabadiliko mapya kulingana na matakwa ya shirika hilo la kimataifa.

Aidha, alisema mikakati mingine ni pamoja na kuendelea utoaji mafunzo kwa ajili ya wakaguzi ili kupata weledi na namna bora ya kufanya kaguzi, usimamizi wa uthibiti wa usafiri wa anga na kufanya kaguzi za ndani kutathimini uwezo wa kampuni zilizosajiliwa nchini kwa kuzingatia matakwa ya kanuni za usafiri wa anga nchini.

"Tunaendelea kusimamia mafunzo endelevu kwa marubani, wahandisi, na watendaji wengine wa sekta ya usafiri wa anga ili tuweze kuongoza katika sekta ya usafirishaji Afrika," alisema Msangi.

Mkurugenzi Mkuu huyo wa TCAA, aliongeza kuwa wanafanya uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya uongozaji wa ndege na mawasiliano kuhakikisha inaendana na mabadiliko ya kiteknolojia.

Katika kuhakikisha mamlaka hiyo inaaminika kimataifa, alieleza wanashirikiana na nchi jirani na mashirika ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kubadilishana uzoefu.

"Tunafurahi kueleza kwamba tunaendelea kuboresha viwanja vya ndege na miundombinu inayohusiana na usafiri huo na inakidhi viwango vya kimataifa," alisisitiza.

Katika majumuisho ya kamati hiyo, wabunge waliutaka uongozi wa TCAA, kusimamia kikamilifu mikakati hiyo na pamoja na kuhakikisha chuo cha CATC kinajengwa kukamilika haraka ili vijana wa kitanzania waweze kupata ujuzi na kuitumikia nchi.

IITA Transforming African Agriculture CGIAR ILRI

**POSITION ANNOUNCEMENT**
**ASSISTANT DATA ANALYST – METEOROLOGICAL AGRICULTURAL**
**IITA-TZ-2025 - R4D-001 -NRS-DSM**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) on behalf of the International Livestock Research Institute (ILRI) invites application for the position of **Assistant Data Analyst – Meteorological Agricultural.**

The **Assistant Data Analyst – Meteorological Agricultural** job is to collate and analyze meteorological and agricultural data to support the ResComm2 project's goals of improving food security and livelihoods in central Tanzania. Additionally, the role involves assisting with coordination and communication tasks and working closely with the project coordinator

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Dar es salaam - Tanzania.

**Roles and Responsibilities:**
- Collect, clean, and analyze meteorological data such as rainfall patterns, temperature variations, and other key factors affecting agricultural activities in central Tanzania.
- Analyze agricultural data including crop yields, soil quality, and farming practices to evaluate the impact of agroecological interventions on smallholder farmers.
- Conduct statistical analysis to identify trends, correlations, and patterns in meteorological and agricultural data, providing insights for the ResComm II project.
- Prepare reports and visualizations to communicate findings, trends, and recommendations based on data analysis to project stakeholders.
- Assist in conducting field surveys, interviews, and on-site data collection activities, ensuring accurate and relevant meteorological and agricultural data are gathered.
- Support coordination and communication within the project team and with external stakeholders
- Perform any other activity as assigned by the national coordinator.

**Qualifications and Experience:**
- A bachelor's degree in meteorology, agriculture, environmental science, statistics, or related field with a minimum of 1 year experience.
- Proficiency in data analysis tools such as excel, R, Python, or specialize packages for meteorological and agricultural data analysis.
- Experience in analyzing meteorological data, and agricultural datasets, and conducting statistical analysis.
- Good communication skills and ability to work collaboratively in a multidisciplinary team.
- Previous experience in analyzing meteorological and agricultural data in the context of development projects is advantageous

**Additional skills:**
- Knowledge of remote sensing technologies and their application in agricultural and meteorological data analysis.
- Experience with Geographic Information Systems (GIS) and spatial analysis for mapping and analyzing environmental data.
- Strong problem-solving skills with the ability to develop solutions based on data analysis.
- Basic project management skills, including the ability to manage timelines and coordinate data collection and analysis activities.
- Ability to work independently and take initiative, demonstrating good organizational and time management skills.

**General information:**
The duration of the contract is two years renewable subject to performance and availability of funds. This is nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

The application pack should include an application letter, copies of certificates, and a curriculum vitae which contains a telephone number, email address, and contact details of two referees. Applications should be sent by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org** and addressed to:

**The Country Representative, IITA-Tanzania,**
**Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road,**
**Mikocheni Industrial Area,**
**Dar es Salaam, Tanzania**

Applicants are requested to include the **reference number for the position** (as indicated on the heading of the announcement) in the subject of their application letter, as well as in the subject of their email. Please note that any applications without the reference number indicated will be automatically disqualified.

**Closing date for applications: Wednesday 29th January2025.** Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

218326002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vitendo vya rushwa ni aibu kwa Jeshi la Polisi, sasa vikomeshwe

**MOJA** ya habari kubwa zilizotikisa juzi na jana katika vyombo vya habari ni askari wawili wa usalama barabarani (trafiki) walioonekana kwenye mitandao ya kijamii wakidaiwa kupokea rushwa kutoka kwa baadhi ya madereva wa mabasi ya abiria, maarufu kama daladala.

Askari hao, kwa mujibu wa video hiyo, walikuwa wanasimamisha mabasi hayo kwa madai ya kukiuka sheria za usalama barabarani katika moja ya vituo mkoani Dar es Salaam. Kwa mujibu wa video hiyo, kila dereva au kondakta aliyekuwa akishuka kutoka kwenye basi, alikuwa akimshikisha askari kitu kinachodhaniwa kuwa ni fedha.

Kutokana na tuhuma hizo, juzi, Jeshi la Polisi kanda maalum ya Dar es Salaam, kupitia Kamanda wake, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, lilitoa taarifa kuwa askari hao wameshakamatwa na wamewekwa mahabusu huku taratibu zingine za kinidhamu, zikiwamo kuhojiwa zikiendelea. Kamanda Muliro alisema hatua za kinidhamu za mashtaka ya kijeshi zimeshaanza kuchukuliwa dhidi yao wakati wakisubiri hatua zingine za kisheria.

SACP Muliro aliongeza kuwa, askari hao walifanya kitendo hicho, wakati wakitekeleza majukumu yao jambo ambalo ni kinyume cha maadili, hivyo kuchafua taswira ya Jeshi la Polisi na serikali.

Kwa ujumla, kama alivyosema Kamanda Muliro, kitendo hicho kimelifedhehesha na kuharibu taswira ya jeshi hilo lililopewa dhamana ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Pia kimethibitisha kwamba madai ya kuwapo kwa rushwa ndani ya jeshi hilo ni ya kweli kwa kuwa askari hao wamefanya hivyo katika mazingira ya uwazi kabisa.

Mara kwa mara, viongozi wakuu wa serikali, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan wamekuwa wakikemea mambo kadhaa yanayoharibu taswira ya Jeshi la Polisi yakiwamo rushwa, kubambikia watu kesi, baadhi ya askari kushiriki katika vitendo vya uporaji wa mali za watu, vifo vya mahabusu mikononi mwa polisi. Madai mengine ni baadhi ya askari kutokufanya majukumu yao kwa weledi kwa kutanguliza maslahi binafsi hasa wakati wa upelelezi wa kesi.


Kuwapo kwa vitendo hivyo, wakati akifugua mkutano wa maofisa wakuu wa polisi mwaka jana, Rais Samia aliagiza jeshi hilo kujitafakari na kumtaka Mkuu wa Jeshi hilo, Inspekta Jenerali Camillus Wambura, kufanya mabadiliko na kuchukua hatua dhidi ya wanaoharibu taswira ya taasisi hiyo nyeti kwa usalama wa raia na mali zao.

Vitendo vya askari wa usalama barabarani na wengine kudaiwa kupokea rushwa vimekuwa vikiimbwa miaka na miaka na hata kuwa sawa na hadithi isiyo na mwisho. Katika miaka kadhaa iliyopita ripoti maalumu ya chombo kimoja cha Habari ilionesha kuwa rushwa na usalama barabarani iko kila kona ya nchi na mfumo uliozoeleka katika maisha.

Aidha, kuota mizizi kwa vitendo hivyo kuwapo kwa madai ya kulindana na pia baadhi ya maofisa wa ngazi ya juu kuwa sehemu ya vitendo hivyo. Kwa maneno mengine, kumekuwa na madai kwamba wakubwa hao hupewa mgawo wa fedha hizo na askari walioko chini yao, hivyo vitendo hivyo kuwa sehemu ya kawaida ndani ya jeshi hilo.

Ikiwa ndiyo kwanza mwaka 2025 umeanza na vitendo hivyo kuonekana hadharani huku video nyingine ikioneshwa kuhusu vitendo hivyo, ni wajibu wa Jeshi la Polisi sasa kuchukua hatua kali dhidi ya askari wanaotuhumiwa au kubainika kujihusisha na mambo hayo. Jeshi lichukue hatua madhubuti zikiwamo kufanya mabadiliko ya askari ndani ya kikosi cha usalama barabarani ambacho ndicho kwa kiasi kikubwa kinahusishwa na tuhuma hizo.

Ni wazi kwamba kama kuna dhamira ya dhati na ya kweli katika kutokomeza vitendo vya rushwa, hasa vikosi na idara zinazohusishwa na mambo hayo, Jeshi la Polisi bila rushwa inawezekana.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kinababa, mshikane mkono na kinamama, tunaona wanavyoweza



Na Tuntule Swebe

**MWANAMKE** ni mama, mzazi ambaye daima ni mlezi wa jamii.

Hivyo, katika nafasi yake anatakiwa kutambua anabaki kuwa mhimili mkubwa katika kupambana na kuimarisha gurudumu la maisha, hata likasonga mbele.

Kila analopitia mwanamke, humzunguka kila mtu likimhusu kwa namna moja au nyingine. Hivyo, wanawake wanapaswa kusimama kwa kuwaongoza wa toto wa kike, ili waweze kutambua nafasi yao na kujua ni kipi kinafaa na kisichofaa, kinachostahili na kisichostahili.

Kwa ujumla wanaangukia wajibu wa kufahamu mambo mtambuka yanayowazunguka.

Familia nyingi za Kiafrika zimekuwa na mtazamo tofauti kuhusu kinamama, wakiwapo wanaoamini nafais yake kuu ni "mfanyaji kazi za nyumbani."

Kwa dhima waliojiwekea katika hilo, kuna matukio ya wanaume hao, hutumia fursa hiyo kuwatumikisha wake zao katika namna isiyofaa, wapo wanaofikia mbali kuwaletea magumu yasiyo na huruma.

Mfano kuna jamii wanaegemea mila kwamba, kinamama hawaruhusiwi kuwa na kauli sehemu yeyote, kwa kutoa hoja zake iwe katika ukoo au kaya mbalimbali.

Mwanamke huyo anashinda nyumbani akitekeleza majukumu yote, baadhi ya mikoa kuna wanaume wanaendelea kutumikisha kinamama, pasipo kujali ama wamechika au la. Hapo mama huyo anaelemewa akikata kuni, kuchota maji, kupika na safari zisizikoma za shambani, ihali mwanaume akiwa amekaa, hoja yake kuu 'yeye ndiye muoaji.' Kuanzia nukta hiyo niliyoishia, kwa uchungu natamka ujumbe huu "

Wanaume, peaneni elimu, mkumbuka kuwa mwanamke ana haki, kwani hata yeye anachoka, hivyo anatakiwa kupumzika."

Hilo ni jambo linalosaidia kuweka usawa kwa wote, wakipeana elimu, juu ya kurithi, siyo suala la mwanamke kuangukia tena mila za baadhi ya makabila wao wakirithi wajane.

Hilo linatokea, pasipo ridhaa zao. Ni muhimu kutambua kua huo ni unyanyasaji na ni makosa kisheria kumgandamiza haki na uhuru wa mwanamke, hivyo ni vyema mkaacha mila hizo.

Mwanamke katika hilo namhimiza kokote aliko, suala hilo la mjane kurithiwa na ndugu limepitwa na wakati.

Nawatia moyo wanawake wenzangu, wajikwamue katika hilo, kwani sheria zipo za kuepuka ukatili huo. Hivyo, mwanaume uliyemrithi mjane chukua hatua kwani sio vyema kumuweka mtu kifungoni kwani anakosa uhuru wa kuongea lolote.

Mwanamke anayo nafasi kubwa katika jamii, anao uhuru wa kushiriki kwenye siasa wakati tunaingia mwaka 2025 wa uchaguzi mkuu.

Hivyo inatupasa kukumbuka kuwapo nafasi ya kuwa wazalendo, tukishiriki kikamilifu kwenye uchaguzi na kuwa wenye maono ya kuwania cheo chochote.

Nanyi kinamama, msiache kuwa na malengo ya kutimiza ndoto zenu, kwani kuna baadhi ya wazazi vijijini wamekuwa na mtazamo tofauti katika malezi ya watoto.

Ninaamini, mtoto hawezi ana haki. Wako sawa katika jamii, huku akiwa na uwezo wa kumsaidia kila mtu.

Pia, tusisahau kuwa, mtoto wa kike anaweza kuikomboa dunia, ni mama wa jamii, pale anapopewa haki, anakuwa na uthubutu wa kukomboa taifa zima. Tujue, watu wote wapewe elimu kua mtoto wakike ni chanzo cha maendeleo na inatupasa kuvikumbuka yombo vinavyotetea haki za wanawake vipo. Kisiasa nako bado hakuko juu sana, ingawa kwetu Tanzania tuna walau rekodi nzuri, tunaye Rais Samia Suluhu Hassan, huku jana tulisikia chama cha ACT Wazalendo, nacho kaibuka

Mwanamama Dorothy Semu, katangaza kuingia kinyang'anyiro cha chama chake, kuwania kupeperusha bendera ya chama chake, akiwania urais.

Bila shaka watoto wa kike walioko shuleni, wana wajibu wa kusoma kwa bidii wakiwa nafasi ya juu zaidi, kuongoza katika fursa mbalimbali.

Bila kusahau kinababa wote, nao wapeane elimu juu ya utambuzi wa nafasi ya mtoto wakike na wakina mama kwa ujumla, taifa letu litazidi kuwa imara zaidi. Niwasihi wanaume wapeni fursa kinamama msiwabane kwani wanayo nafasi kwenye ngazi za familia na kisiasa.

# TRA yawapa elimu wapangaji kukata 10% ya pango

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetoa elimu ya mpangaji wa nyumba anavyotakiwa kukata sehemu ya kodi kabla ya kumlipa mwenye nyumba na kulipa kwa mamlaka hiyo kama sehemu ya kodi ya zuio la pango.

Ofisa Mwandamizi wa kodi Mkoa wa Kikodi Kariakoo, Mashenene Benny, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Kodi, mpangaji wa nyumba anapaswa kumkata mwenye nyumba asilimia 10 kabla ya kumlipa malipo yake ya kodi ya pango.

Benny, alisema kodi hiyo kisheria inajulikana kama kodi ya zuio la pango ambalo baada ya kuikata kwa mwenye nyumba anatakiwa aipeleke TRA.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam, wakati akitoa semina kwa viongozi wa serikali za mitaa Kariakoo, kuhusu sheria za pango za nyumba.

"Kodi ya zuio la pango ni kodi ambayo inapaswa ilipwe na mwenye nyumba, kwa sababu kisheria mpangaji anapomlipa mwenye nyumba anatakiwa azuie asilimia 10 ya malipo yake kwa mwenye nyumba huyo," alisema Benny.

"Kodi ya zuio la pango ni kodi ambayo inatokana na biashara ya kupangisha, kwa hiyo mwenye nyumba anapompangisha mtu, mpangaji anatakiwa azuie asilimia 10 ya malipo anayolipa kwa mwenye nyumba huyo kwa sababu kisheria inatakiwa ilipwe kwa Mamlaka ya Kodi."

Kadhalika, alisema si kwa nyumba ya kupanga kwa ajili ya kuishi pekee ndio inatakiwa kukatwa asilimia 10 ya zuio la pango, bali hata kwa anayepanga kwenye flemu ya biashara.

"Kwa mfano ikitokea labda mpangaji amepanga flemu ya duka kwa mwenye nyumba, na analipa Shilingi milioni moja kwa mwezi na halafu mkataba wao ni wa miezi mitatu, hivyo katika kiasi cha Shilingi milioni tatu, anatakiwa kukata Sh.300,00 kama kodi ya zuio la pango akamlipa Sh. 270,000 pekee na hiyo inayokatwa inapelekwa TRA," alifafanua Benny.

Alisema tatizo kubwa linalochangia watu kushindwa kutekeleza hayo ni kutokujua sheria na TRA wataendelea kutoa elimu kuhusu kodi mbalimbali ili kila mtu atimize wajibu wake.

Pia, alisema eneo jingine ambalo bado kuna shida ya uelewa ni namna ya kulipa kodi inayotokana na uuzaji wa ardhi na kwamba kifungu cha 90(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, kinaeleza kuwa, kama mtu anapata faida kwa kuuza ardhi au jengo lake, anatakiwa alipe asilimia 10 ya faida kama kodi.

"Hii italipwa kama kutakuwa na uthibitisho wa gharama za ujenzi, na gharama nyingine zinazohusiana na jengo na kama hakutokuwa na uthibitisho wa gharama, basi kodi itakuwa ni asilimia tatu ya thamani ya ardhi au jengo lililouzwa," alisema Benny.

Aliwataka viongozi wa mitaa kushirikiana na Mamlaka hiyo kutekeleza sheria hiyo ya kodi ya majengo na ardhi hususani wanaposhiriki katika upangaji au kwenye mauziano wa ardhi.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, mkoani Morogoro Khamis Katimba akizungumza kwenye kikao cha uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi la Wilaya hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaihakikishia IMF fedha inazotoa kukuza uchumi wa nchi

**Na Waandishi Wetu,**

DODOMA

SERIKALI imesema kuwa itaendelea kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na kuhakikisha fedha zote za maendeleo zinazotolewa zinatumika kukamilisha azma ya kukuza uchumi wa nchi.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo jijini Dodoma wakati akimuaga Kiongozi wa Timu ya Wataalam ya IMF kwa Tanzania, Charalambos Tsangarides, aliyemaliza muda wake baada ya kuhudumu kwa zaidi ya miaka mitatu na nusu.

Alisema serikali itaendelea kutekeleza dhamira yake ya kuwaletea wananchi maendeleo na kukuza uchumi kwa ujumla kupitia juhudi mbalimbali inazofanya ikiwamo kutafuta fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati.

"Kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kujitolea kwako katika kusaidia safari ya maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu, ninawahakikishia kwamba timu yangu itawapa ushirikiano wote unaohitajika, kwa upande mwingine, nina furaha kuwajulisha kwamba tunaendelea vyema na hatua zetu za mageuzi chini ya programu mpya ya serikali ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia dirisha la Resilient and Sustainable Fund (RSF)," alisema Dk. Nchemba.

> **"Kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kujitolea kwako katika kusaidia safari ya maendeleo ya kiuchumi**

Aidha, alimkaribisha kiongozi mpya anayechukua nafasi hiyo, Nicolas Blancher na kumuahidi ushirikiano kutoka Serikali ya Tanzania.

"Napenda kuchukua fursa hii kumkaribisha rasmi Nicolas Blancher, kama kiongozi wetu mpya wa 'Mission' kwa Tanzania na tunafurahi kupata nafasi ya kushuhudia mwongozo kutoka kwa mtaalamu mwingine kama tulivyofanya na kiongozi anayemaliza muda wake katika kufanikisha maendeleo yetu endelevu ya kiuchumi," alisema Dk. Nchemba.

Tsangarides, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano mkubwa alioupata wakati akitekeleza majukumu yake nchini.

Aidha, ameipongeza serikali kwa juhudi za kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kuahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania kuimarisha ustawi wa wananchi wake hata baada ya kumaliza muda wake wa kuhudumu.

Kiongozi mpya wa Timu ya Wataalam ya IMF, Blancher ameahidi kushirikiana kikamilifu na serikali na kumhakikishia Dk. Nchemba kuwa ataendeleza ushirikiano na kazi zilizofanywa na mtangulizi wake huku akisisitiza dhamira ya kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanatimia.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Meya atishia kujiuzulu kisa tuhuma za rushwa watumishi

**Na Benny Kingson,**
TABORA

MEYA wa Halmashauri ya Tabora, Ramadhani Kapela, amesema yuko tayari kujiuzulu iwapo baadhi ya maofisa wa idaya ya ujenzi wa halmashauri hiyo wanaotuhumiwa kula rushwa ya Sh. milioni 20.7 watalindwa na viongozi wa serikali.

Maofisa hao wanatuhumiwa kuhusika na rushwa hiyo ambayo ni ya malipo ya vibali vya ujenzi wa majengo, hivyo kuisababishia manispaa kupoteza mapato.

Kapela alisema hayo kikao cha kupitisha rasimu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 kwa manispaa hiyo ya Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na kumwagiza mkurugenzi wa halmashauri hiyo kushirikiana na vyombo vya dola, kuchukua hatua stahiki.

Alisema yuko tayari kujiuzulu nafasi yake endapo wahusika hawatachukuliwa hatua za kisheria hata kama wanafahamiana na viongozi wakuu wa serikali, akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo anachotaka ni haki kutendeka kwa kuwa watuhumiwa wamekuwa wakifanya hivyo kwa makusudi bila kuogopa.

"Naomba niweke wazi kuwa niko tayari kujiuzulu nafasi yangu endapo hawa wahusika hawatachukuliwa hatua za kisheria. Kama watalindwa mimi naachia ngazi. Mkurugenzi na vyombo vya dola washughulikieni hawa na mkishindwa mtawajibishwa," alisema.

Suala hilo limeonekana kuwakwaza madiwani wa manispaa hiyo na kuunga mkono kauli na maagizo ya Mstahiki Meya.

Aidha, Katibu wa CCM Wilaya ya Tabora, Daniel Mhina, alikemea baadhi ya wafanyabiashara na wawekezaji wanaokwepa kulipa kodi na kuanza kuomba msaada kwa njia za panya kutoka kwa viongozi wa chama na serikali.

Mhina alisema inasikitisha kuona watumishi walioaminiwa na serikali wanaingia katika tuhuma za rushwa na kusababisha manispaa kukosa mapato huku wahusika wakijineemesha jambo hilo ambali kwa mujibu wa kiongozi huyo, haliwezi kuvumiliwa.

Siku chache zilizopita, kuliripotiwa kuwapo na malalamiko kutoka kwa Umoja wa Madereva Mkoa wa Tabora (UWAMATA) wakiwashutumu baadhi ya watumishi wa manispaa hiyo kuchukua pesa kwa watu na kuwaruhusu kujenga vibanda kwenye eneo la kituo cha magari yaendayo Sikonge, Uyui na Urambo, maarufu kama Maduka 30.

Uchunguzi ulibaini kuwapo kwa vibanda hivyo ambavyo vimejengwa na kuendelea kujengwa kila kukicha na kusababisha kupungua eneo la kituo hicho kinachokadiriwa kuhudumia magari kati ya 50 na 70. Madereva hao walidai kuwa wamekuwa wakilipa ushuru lakini hawatendewi haki ikiwa ni pamoja na kufanyiwa maboresho ya miundombinu.

Kutokana na ujenzi wa vibanda hivyo, kuna hatari ya kutokea majanga ya moto hasa baada ya kushamiri kwa vibanda vya mama lishe wanaopika kituoni hapo.

Hali hiyo pia ni hatari kwa usalama wa magari, watu na mali zao na inaonesha kuwa wahusika hawaoni hayo yote kwa kuwa kuna viashiria vya kuwapo kwa vitendo vya rushwa.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Elias Kayandabila, alipoulizwa kuhusu hayo, alisema amepokea taarifa japo yuko likizo licha ya kwamba alisema yeye ndiye chanzo cha yote na kwamba amekuwa akiibua moja baada ya lingine na atasimamia, kutekeleza maagizo yote na kuchukua hatua stahiki haraka.



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Muhoji, jimbo la Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiwa na madawati waliyonunua kijijini hapo juzi, kwa ajili ya watoto wao wanaotarajia kuanza kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya kijiji hicho mwezi ujao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti utatifi CBE zawekwa majarida kimataifa

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimesema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ripoti 288 za utafiti zilizofanywa na watalamu wake, zimewekwa katika majarida ya kimataifa kutokana kuandaliwa kwa viwango vya kimataifa.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa chuo hicho.

Kwenye maadhimisho hayo yanayotarajiwa kufanyika wiki ijayo kampasi kuu ya chuo hicho, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, pamoja na wageni mashuhuri zaidi ya 300.

Prof. Lwoga alisema mafanikio ya ripoti za utafiti wake kuchapishwa kwenye majarida ya kimataifa kumetokana na CBE kujenga ushirikiano na taasisi za kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha utafiti unakuwa wa ubora wa hali ya juu na wenye ushawishi mkubwa.

Alisema chuo hicho kimekuwa kikishirikiana na taasisi na vyuo mbalimbali vya nje ya nchi hali ambayo imekifanya kupata uzoefu na ujuzi wa kukiwezesha kuboresha mitaala yake na kuongeza idadi ya wanafunzi mwaka hadi mwaka. Alisema ndani ya miaka hiyo 60 chuo kimefanikiwa kuzalisha maelfu ya wahitimu wa fani mbalimbali ambao wanauwezo wa kujiajiri na kuajiri wenzao badala ya kuhangaika kutafuta ajira mara baada ya kuhitimu. Alisema katika miaka ya hivi karibuni chuo kilifanikiwa kuanzisha program ya uanagenzi na program atamizi ambazo zimekuwa msaada mkubwa wa wahitimu wa chuo hicho kujiajiri na kufanyabiashara kwa ufanisi wanapohitimu chuoni hapo

Akizungumzia maadhimisho hayo yatakayofanyika wiki ijayo, Profesa Lwoga alisema kuwa CBE iliyoanzishwa mwaka 1965, kufuatia makubaliano ya ushirikiano kati ya serikali za Tanzania na Ujerumani imekuwa na mafanikio makubwa.

Prof. Lwoga alisema maadhimisho hayo yataambatana na shughuli nyingine mbalimbali ikiwemo kusaini hati za makubaliano kati ya Chuo na wadau mbalimbali, uzinduzi wa Dira ya Miaka 50 ya Chuo, Ugawaji zawadi kwa watu maalum, kukata cake pamoja na burudani.

Alisema tangu kufunguliwa rasmi na Rais wa kwanza, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, CBE imekuwa mstari wa mbele katika utoaji wa elimu bora ya biashara, kukua na kuboresha huduma zake kuendana na mahitaji ya soko.

Alitaja maeneo yaliyoboreshwa kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya kampasi na wanafunzi ambapo Chuo kilianza na Kampasi moja ya Dar es salaam na idadi ya wanafunzi 30 tu ambapo hivi sasa kina Kampasi nne na idadi ya wanafunzi imeongezeka maradufu.

Alisema kwa sasa kampasi ya Dar es salaam ina wanafunzi wanafunzi 14,536, Dodoma iliyoanzishwa mwaka 1983 ina wanafunzi 4,611, Mwanza ilianzishwa 2007 idadi ya wanafunzi 2,098 na Mbeya ilianzishwa 2013 ina wanafunzi 1018 na kwamba hiyo inafanya jumla ya wanafunzi kwa Chuo kizima kufikia 22,263.

## Wakubaliana kuchangia chakula cha watoto wao

**Na Sabato Kasika**

WAZAZI wa wanafunzi wanaotarajia kuanza kidato cha kwanza katika sekondari mpya ya Kijiji cha Muhoji, Musoma mkoani Mara, wamekubaliana kuchangia chakula cha mchana kwa watoto wao.

Uamuzi huo wa kuchangia chakula ulifikiwa katika kikao kilichofanyika juzi kijijini hapo chini ya uongozi wa kijiji hicho na viongozi wao akiwamo mtendaji wa Kijiji, Samwel Owino.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo, kila mzazi au mlezi atachangia kilo nane za unga, mahindi au mtama na wengine maharage kwa ajili ya kufanikisha mkakati huo wa kuwapo chakula cha mchana shuleni kila baada ya miezi sita.

"Wazazi pia wamekubaliana kuchangia ununuzi wa madawati ambayo yanatengenezwa hapa kijijini na tayari yameshapatikana 34. Kila mzazi au mlezi anachanga Sh. 65,000 za kununua madawati," alisema Owino.

Alisema wamekubaliana pia kujenga uhusiano mzuri kati yao na walimu na wataendelea kushirikiana vizuri na serikali ili sekondari yao ili iwe mfano wa kuigwa katika ubora wa elimu.

"Kijiji chetu kina wakazi 1,526 lakini wale wanaochangia maendeleo ni 441 kwani kwa kawaida katika sensa, mara nyingi idadi kubwa ya watu huwa ni wale wa umri wa chini ambao hawajajitegemea," alisema.

Owino alisema sekondari hiyo inatarajiwa kufunguliwa Februari mwaka huu ikiwa na wanafunzi 60 wa kidato cha kwanza, madarasa manne, vyoo matundu 13 na kwamba suala la idadi ya walimu, wanasubiri uamuzi wa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo alisema ujenzi wa sekondari hiyo ulianza Desemba mwaka 2022 baada ya wananchi kuazimia kwa kauli moja kujenga sekondari ya kijiji chao. Prof. Muhongo alisema walifikia uamuzi huo ili kuwapunguzia watoto wao kutembea umbali mrefu kwenda kusoma katika sekondari ya kata iliyopo Kijiji cha Bugwema.

"Baada ya uamuzi huo, nilifanya harambee ya kufanikisha ujenzi huo, kila kaya ilikubali kuchangia shilingi 75,000, ngu-vukazi kwa ajili ya kusafisha eneo la kujenga shule, kuchimba msingi na kusomba mchanga," alisema Prof. Muhongo.

Mbunge huyo alisema serikali kuu nayo imetia mkono katika ufanikishaji wa ujenzi wa sekondari hiyo kwa kutoa Sh.milioni 75 ambazo zimesaidia kusukuma mbele maendeleo ya ujenzi huo.

Musoma Vijijini tuna kata 21, sekondari 26 za kata na mbili za binafsi. Sekondari mpya sita zimepagwa kufunguliwa mwaka huu. Matayarisho ya kuanza ujenzi wa sekondari nyingine sita yamekamilika," alisema. Mmoja wa wazazi, Patti Mussa, alisema watoto wao walikuwa wakitembea umbali wa kilomita 10 kfuata elimu Bugwema Sekondari ndipo wakaamua kujenga ya kijiji chao.

"Wakazi wa Muhoji tuna mwamko wa elimu, ndio maana tumejitolea kujenga sekondari ya kijiji chetu. Lakini pia tunashukuru mbunge kwa kuchangia ujenzi wa sekondari jimboni mwake," alisema Mussa.

Mussa alisema anatamani kuona wanafunzi watakaoanza masomo katika sekondari hiyo wanafanya vizuri katika masomo ili wafike juu zaidi ili kukitangaza kijiji hicho.

# Serikali yamaliza mgogoro wa uchimbaji madini

**Na Godfrey Mushi,** SIMANJIRO

HATIMAYE serikali imeumaliza mgogoro wa mpaka wa leseni ya uchimbaji wa madini aina ya tanzanite kati ya kampuni mbili za uchimbaji wa vito za Njake na Miroshi, zilizokuwa zikigombana katika eneo la Mirerani, Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara.

Akitangaza kumalizika kwa mgogoro huo, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema amelazimika kuzikutanisha pande hizo mbili ili kuwasikiliza na kisha kutafuta ufumbuzi wa kudumu juu ya mgogoro huo.

"Baada ya kupokea taarifa ya timu ya wataalamu niliyoiunda kuchunguza mgogoro huu, naelekeza baada ya pande zote mbili kuridhia, kila mmoja sasa arejee kwenye eneo la mipaka ya leseni yake; na kampuni ya Njake imfidie Miroshi, gharama alizoingia awali za uchimbaji.

**"Hii ina maana kwamba kila mmoja aendelee na uchimbaji katika eneo la leseni yake kwa amani."**

"Hii ina maana kwamba kila mmoja aendelee na uchimbaji katika eneo la leseni yake kwa amani."

Kikao hicho cha usuluhishi, kilihudhuriwa na viongozi wa wizara, akiwemo Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Yahya Samamba na Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini Tanzania, Ramadhani Lwamo.

Aidha, Waziri Mavunde, aliwataka wachimbaji kote nchini kuhakikisha wanazingatia sheria na kanuni ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

"Serikali inatamani kuona sekta ya madini inaendelea kukua na kutoa mchango wa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, migogoro siku zote inaturudisha nyuma katika jitihada za kuongeza uzalishaji na kuchochea uchumi.

...Ni maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwamba tufanye utatuzi wa haraka wa migogoro kwenye sekta ya madini ili kuchochea ukuaji wake." alisema

Kutokana na maelekezo ya Rais Samia, Waziri Mavunde aliwataka wachimbaji wote kuzingatia sheria katika shughuli zao za kila siku.



Mkuu wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Emmanuela Kaganda (kulia), akikabidhi mahitaji ya shule kwa wanafunzi kutoka familia zisizo na uwezo, wilayani humo juzi, ili waweze kurejea mashuleni. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Mtendaji wa Kijiji kortini tuhuma ubadhirifu

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

ALIYEKUWA Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ruvu Remit kilichopo Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Denis Mazigo, amefikishwa katika mahakama ya wilaya hiyo akikabiliwa na makosa mawili ya matumizi mabaya ya madaraka na ubadhirifu.

Mazigo alifikishwa mahakamani humo jana na kusomewa mashtaka hayo mbele ya hakimu wa mahakama hiyo, Onesmo Necodemo.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Faustin Mushi, akisoma hati ya mashtaka, alidai kuwa mshtakiwa katika kosa la kwanza la matumizi mabaya ya madaraka, anashtakiwa kinyume cha Kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Ikisomwa pamoja na kosa la ubadhirifu, ambalo ni kinyume na Kifungu cha 28 (1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022; vyote vikisomwa pamoja na aya ya 21 Jedwali la 1, Kifungu cha 57 (1), 60(2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupanga, Sura 200 kama ilivyofanyiwa marejeo Mwaka 2022.

Aliendelea kudai kuwa, katika shauri hilo la uhujumu uchumi, namba ECC.1050/2025, kwa nyakati tofauti, mshtakiwa akiwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ruvu Remit, alikusanya faini Sh. 750,000 kutoka kwa wajumbe 15 wa serikali ya kijiji hicho, kwa makosa ya kutokuwa na vyoo katika kaya zao na kisha akatumia fedha hizo kwa matumizi yake binafsi.

Mshtakiwa huyo baada ya kusomewa mashtaka hayo, alikana makosa yote mawili.

Baada ya kukana, hakimu Necodemo alisema dhamana iko wazi kwa mshtakiwa.

Mshtakiwa Mazigo alikamilisha masharti ya dhamana na hakimu Necodemo, alimpa dhamana baada ya kuwa na mdhamini mmoja ambaye ni mtumishi wa umma, na kitambulisho chake pamoja na kusaini bondi ya shilingi milioni mbili.

Shauri hilo litatajwa tena mahakamani humo, Februari 6 mwaka huu, kwa kuanza kusikiliza mashahidi wa upande wa mashtaka.

# Wanafunzi 4 wakatisha masomo sababu ujauzito

**Na Mary Mosha,** SAME

WANAFUNZI wanne wanaosoma shule za msingi na sekondari katika Kata ya Kalimawe na Bendera wilayani Same mkoani Kilimanjaro, wamekatisha masomo yao baada ya kupata ujauzito.

Mkuu wa wilaya hiyo, Kasilda Mgeni, alisema matukio ya kuwapa mimba wanafunzi yanaua ndoto za watoto wa kike na juhudi za serikali katika kuinua kiwango cha elimu kwa wasichana.

Mgeni alikuwa akizungumza jana na wakazi wa kata hizo, alipokwenda kusikiliza na kutatua kero mbalimbali.

"Nimekuja hapa kuhamasisha wazazi na walezi, kuwapeleka watoto shule wanaoanza chekechea, darasa la kwanza na waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza ili kufanikisha ndoto zao.

"Ndugu zangu kama mnavyojua serikali imeboresha mazingira ya elimu kwa wanafunzi wote, hasa wa kike. Sasa nasikia kuna wanne wamepata mimba.


"OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), naagiza hakikisha wahusika wa matukio haya wanakamatwa mara moja na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Zaidi alifafanua, "Tunahitaji msaada wa jamii kukemea na yenyewe vitendo kama hivi ambavyo havikubaliki. Haiwezekani kwa sababu vinaharibu maisha ya watoto wetu na kukiuka maadili yetu kama Watanzania."

Kutokana na vitendo hivyo, amewataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuhakikisha watoto wanalelewa kwa maadili mema na kulindwa dhidi ya vitendo vya ukatili, vinavyoathiri maendeleo yao ya kielimu.

"Hata wazazi walioshirikiana na wanaume waliowapa mimba wanafunzi kwa kupokea kitu kidogo nao hawatapona. Nimeagiza nao watafutwe na washitakiwe kwa kosa la kuficha wabakaji," alisema.

Kwa upande wao baadhi ya walimu wakuu wa shule hizo wameeleza kuwa changamoto kubwa ni ushirikiano mdogo kutoka kwa wazazi wa waathirika, ambao mara nyingi huficha ukweli na kuweka vikwazo katika upatikanaji wa ushahidi wa kisheria.



# Vitambulisho machinga vyarejeshwa kivingine Maswa

**Na Alex Sayi,** MASWA

MWANASHERIA wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Fredrick Mussa amesema serikali imekuja na utaratibu mpya wa kuwatambua wafanyabiashara wadogo 'machinga' kupitia vitambulisho vilivyofanyiwa maboresho.

Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe na kueleza kuwa vitambulisho hivyo ni vilevile vya zamani lakini kwa sasa vimefanyiwa maboresho muhimu ikiwa ni pamoja na kubeba taarifa zote muhimu za mfanyabiashara.

“Katika kitambulisho hicho kinachosajiliwa kwa gharama ya Sh.20,000, mfanyabiashara atasajiliwa katika mfumo na taarifa zake zote muhumu na kitadumu kwa miaka mitatu, kitawawezesha kupata mikopo katika taasisi mbalimbali ili kuinua mitaji yao,” alisema Mussa.

**“Katika kitambulisho hicho kinachosajiliwa kwa gharama ya Sh.20,000, mfanyabiashara atasajiliwa katika mfumo na taarifa zake zote muhumu na kitadumu kwa miaka mitatu, kitawawezesha kupata mikopo...**

Baadhi ya wafanyabiashara wilayani hapa akiwemo Mwenyekiti wa Soko Kuu la Wilaya, Nashoni Naftari alisema maboresho ya kitambulisho hicho yatawasaidia kudhaminika na taasisi mbalimbali za mikopo zikiwemo benki.

Kadhalika alisema wafanyabiashara sokoni hapo wamefurahishwa na maboresho hayo licha ya kuwa kitamburisho hicho hakitaondoa tozo za halmasauri sokoni hapo kama ilivyokuwa kile cha awali.

Ofisa Uhusiano wa NMB, Ezekiel Shikobe alisema wameingia ubia na serikali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara hao na kuwa tayari serikali imeshaingiza fedha hizo benki tayari kwa kuwakopesha wafanyabiashara hao.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro (kulia), akizungumza wakati akisikiliza na kutatua kero mbalimbali za wanakijiji cha Mwang'halanga, wilayani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC aagiza viongozi kutatua kero za wananchi

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MKUU wa wilaya ya Tarime, Edward Gowele amewataka viongozi na watumishi wa umma kuhakikisha wanawahudumia wananchi ipasavyo na kutatua kero zinazowakabili katika maeneo yao.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na vikundi vya vijana, wanawake na wenye ulemavu katika Kata ya Nyakonga na kueleza kuwa baadhi ya viongozi wameshindwa kutafuta majibu ya kero za wananchi.

"Lazima tutumie ubunifu katika nafasi zetu na rasilimali kidogo tulizonazo kama viongozi na watumishi kutatua kero za wananchi haraka iwezekanavyo kuliko kulazimika kusubiri mgawo kutoka serikalini katika maeneo yetu," alisema.

Aidha, katika mkutano huo Gowele alikabidhi Sh.milioni 17 ya msaada binafsi iliyotolewa na Diwani wa Kata hiyo Simon Kiles kwa lengo la kuwasaidia mitaji ili kujiinua kiuchumi.

Pia, alimpongeza diwani huyo kwa kujitolea kujenga ofisi ya kata pamoja na kuchangia fedha kuwezesha vikundi vya kilimo na vijana ambapo aliwataka wawakilishi wengine wa wananchi kuiga mfano wake.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Simon Kiles alisema licha ya fedha kwa makundi hayo vilevile amevipatia msaada vikundi vya kilimo kwa kuwapatia pembejeo za kilimo bure katika misimu miwili ya kilimo iliyopita ili kuboresha shughuli zao za kilimo na kuongeza uzalishaji.

"Tunajaribu kuwajengea uwezo vikundi vya wananchi kuzalisha mali ikiwemo mazao ya kilimo na hivyo kuwezesha kujitegemea bila kusubiri fedha kutoka serikalini ambazo hazitoshi kuhimili mahitaji ya kila mtanzania," alisema Kiles.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Tarime, Sauli Mwaisenye aliwataka wananchi kutafuta ushauri wa wataalamu wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kila siku ya uzalishaji mali katika kilimo na biashara ili kupata matokeo bora na kuinua maisha yao.

"Tunawashauri wataalamu wetu katika idara zote za halmashauri kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi hasa vijijini juu ya kutekeleza shughuli za uzalishaji ikiwemo kilimo bora na ujasiriamali kupitia vikundi vya wananchi," alisema Mwaisenye.

# Soko la ushindani kudhibiti utoroshaji madini ya bati

**Na Mohab Dominick,** KYERWA

SERIKALI imedhamilia kuweka soko la ushindani la madini ya bati wilayani Kyerwa mkoani Kagera, ili kudhibiti utoroshaji madini unaotajwa kufanywa na wachimbaji.

Ofisa Madini Mkazi Wilaya ya Kyerwa, Dotto Ernest, alisema hayo katika sherehe za kadhimisha mwaka mpya kwa wachimbaji wa madini hayo.

Alisema madini hayo yanatakiwa kulipiwa kodi kama yalivyo mengine na siyo kutoroshwa na kuvushwa mipaka kwenda nchi jirani ya Rwanda kutokana na kukosa soko la ndani.

Ernest alisema watoroshaji wa madini hayo wanatambuliwa na wanashirikiana nao katika shughuli mbalimbali, hivyo kuwataka wachimbaji hao kuhakikisha wanashiriki kuzuia hali hiyo ili serikali ipate mapato na kuwahudumia wananchi.

“Tutaweka soko la ushindani soko la tin ili kuepusha utoroshaji wa madini hayo jambo ambalo linasababisha serikali kukosa mapato na kufaidisha nchi jirani ya Rwanda ambayo haina madini hayo,” alisema Ernest.

Alisema serikali itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wote watakaobaini kutorosha madini hayo kinyume cha sheria na kuwa hawapo tayari kuvumilia vitendo hivyo.

“Acheni kupeleka madini ng’ambo nawaomba wachimbaji wa wa madini ya bati fuateni sheria na taratibu za serikali ikiwa pamoja na usalama wakati mnapokuwa kazini na serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwenu,” alisema.

Kadhalika, aliwataka vibarua wote wanaoingia kutoka nchi za jirani kwa ajili kushughulika na uchimbaji kuhakikisha wanafuata sheria na taratibu za kuingia nchini.


Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Kagera (KAREMA), Sara Rusambagura aliwataka wachimbaji kuhakikisha wanafanya kazi kwa ushirikiano ili kutimiza malengo ya kundi hilo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, Bahati Eneriko aliwataka wachimbaji wa mdaini kuhakikisha wanafanya kazi kwa malengo na kufuata mifumo ya fedha itakayowasaidia kuwekeza fedha kwa ajili ya maisha yao ya baadaye.

Kaimu Katibu wa wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kagera, Angelius Kamugisha alisema mwenyekiti wa chama hicho ambaye ni Rais Samia Suluhu Hassan anatambua mchango wa wachimbaji wote nchini na anaendelea kuhakikisha anatatua kero zinazowasibu.

Hivyo, aliwaomba wachimbaji hao kuwa wamoja katika shughuli zao hasa wakati soko la ushindani litapokuwa limeanza katika eneo hilo pamoja na wale wanaopata madini hayo ya bati wasiuze kiujanja ujanja kwani watadharauliwa.

Alisema: “Kwa sasa katika eneo hili kuna mahitaji mengi ikiwa ni pamoja na zahanati, maji, vituo vya afya na hivyo kwa kutumia madini hayo ya bati ni utajiri mkubwa kwa wananchi wa eneo hili na yatasaidia kwa kiasi kukubwa kupunguza kero zilizopo”.




Tunaua utalii wetu, kugeuza wanyamapori matahira!

Ukurasa 13



Ukurasa 12

## Gavana BOT: Tunajimudu kiuchumi, akiba fedha kigeni zinawezesha ununuzi wa miaka minne



# Simulizi undani wa biashara dawa kulevya unavyochafua sekta nchini

**Na Zanura Ibrahim**

**WIKI moja na nusu imepita, Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini (DCEA), ilitoa taarifa ya mzigo mkubwa wa dawa za kulevya, ulioweka rekodi kimataifa, raia wa kigeni na meli yao wakinaswa na sasa wameshafikishwa mahakamani, ikiwa na athari za kiafya, kijamii na mwenendo wa kibiashara nchini. Je undani wa biashara hizo kitaifa na kimataifa ni upi? Fuatilia undani wake kibiashara.**



Mzigo wa dawa za kulevya ulionaswa nchini, ukisafirishwa na jahazi kigeni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

HADI sasa nchini, sera na mwenendo wa kiserikali nchini, ikiwamo dhamira iliyomo katika zama za Awamu ya Sita, ni kuhuisha, pia kupaisha biashara za haki.

Na mwenendo wowote ule, katika tafsiri hiyo ya kihistoria, iko katika vita vikali dhidi ya yaliyo haramu, ama kwa mwenendo au aina ya bidhaa husika. Kunakuwapo na mpambano kutoka serikalini kuikabili hali hiyo.

Kuna eneo mojawapo, ambalo kitaifa na kimataifa, nchi iko katika vita vikali navyo katika namna endelevu; biashara ya dawa za kulevya, matendo yanayofanyika kitaifa na kimataifa.

Biashara hiyo, undani wake ni hali inayowahusisha raia wa nchi husika, kwa kushirikiana na magenge ya kihalifu kimataifa, bara Afrika ni sehemu ya waathirika wakuu.

Wasifu wake ni biashara haramu inayohusisha uzalishaji, usafirishaji, na uuzaji wa dawa za kulevya kama vile heroini, kokaini, bangi na dawa za kemikali kama methamphetamine.

Biashara huwa haziishi kuvuruga uchumi kitaifa, panakohusika, huku ikichochea ongezeko la uhalifu, kudhoofisha mifumo ya kiusalama, na kuathiri afya na ustawi wa wananchi wake.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODc) Kupitia taarifa yake ya mwaka 2021, inasema, Afrika imekuwa njia kuu ya usafirishaji wa dawa za kulevya kutoka Amerika Kusini na Asia kuelekea Ulaya na Amerika Kaskazini.

Hiyo inatajwa, kuchangiwa na mambo mbalimbali, ikiwamo udhaifu wa mifumo ya udhibiti, umaskini na ufisadi katika taasisi za umma.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa nchi kama Nigeria, Afrika Kusini, Kenya na Tanzania, zimeorodheshwa kuwa vituo muhimu katika mtandao wa biashara hii haramu.

Mamlaka ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Sheria za Dawa za Kulevya, kupitia ripoti yake ya mwaka 2020, inasema (NDLEA) Nigeria ni moja ya nchi zinazojulikana kwa kiwango kikubwa cha usafirishaji wa dawa za kulevya.

Pia, ripoti hiyo inataja magenge ya kihalifu katika nchi hizo yanahusika kusafirisha dawa za kokeini na heroini kutoka Marekani Kusini na Asia kupitia Afrika Magharibi kwenda Ulaya na Amerika.

Hata hivyo, unatajwa ufisadi kuwapo katika taasisi za serikali na udhaifu wa sheria za kudhibiti dawa za kulevya umechangia kuimarisha biashara hii haramu.

**NJIA AFRIKA MASHARIKI**

Ripoti hiyo ya UNODC, 2021 inasema nchi za Afrika Mashariki hususani Kenya na Tanzania, zimekuwa njia kuu za kusafirisha heroini kutoka Afghanistan kupitia Bahari ya Hindi.

Inaelezwa kuwa, kuna namna bandari ya Afrika mashariki, kuhusika mara kadhaa katika uvushaji dawa hizi za kulevya.

Hiyo inatajwa, kuhusishwa na mikoa ya ukanda wa Pwani inayotajwa kuwa na kiwango zaidi cha matumizi ya heroini, kuashiria tatizo kubwa la afya ya umma.

**TAARIFA YA NCHINI**

Mnamo siku ya Januari 9, kwa maana ya wiki moja na siku kadhaa zimepita, Kamishna Jenerali mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya(DCEA), Aretas Lyimo, akawasilisha taarifa ya udhibiti wa dawa za kulevya ulivyokuwa mwaka jana.

Anasema katika operesheni iliyofanyika mwishoni mwa mwaka uliopita, ulihusisha ukamataji wa kilo 673.2, dawa za methamphetamine na heroin. Anasema, kati yake 448.3 ziliwahusisha raia wanane ku-

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

# Gavana BOT: Tunajimudu kiuchumi, akiba fedha kigeni zinawezesha ununuzi wa miaka minne

**Na Halfani Chusi**

SIKU chache zilizopita, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imewaonya wanaotumia fedha za kigeni, kufanya miamala nchini, ikisisitiza kufanya hivyo ni kuhujumu uchumi wa nchi na ni kosa kisheria.

Ikaongeza kuwa, Kikao cha Kamati ya Sera ya Fedha, kimeamua kuendelea na kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) cha asilimia sita kwa benki za kawaida katika robo ya kwanza ya mwaka 2025.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, anasema mtu anapofanya miamala ndani ya nchi, anatakiwa kutumia shilingi za kitanzania,vinginevyo yuko kinyume akihujumu uchumi wa nchi, kwa sababu anatumia shughuli za uchumi wa Tanzania kwa kutumia sarafu za nchi nyinginezo.

Kuhusu hatua ya kutobadili riba akasema, unalenga kuhakikisha kiwango cha ukwasi kinaendelea kuwa cha kutosha katika uchumi, kudhibiti mfumuko wa bei kubaki chini ya lengo la asilimia tano.

Anataja hilo linawezesha kuongezeka kwa kasi ya ukuaji uchumi kufikia wastani wa asilimia 5.7 katika robo ya kwanza ya mwaka huu.

Gavana Tutuba akafafanua kwamba, ni uamuzi unaolenga kuweka utulivu wa thamani ya shilingi, dhidi ya fedha za kigeni, ili kuendelea kukabili mfumuko wa bei ubaki katika kasi ndogo, hali inayochangia jitihada za kuwafanya wananchi kutofanya miamala yao kwa kutumia fedha za kigeni nchini.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa dunia, Tutuba, anasema kamati hiyo imebaini kuwa ripoti zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia, zinaonesha ukuaji uchumi unakadiriwa kuwa imara katika mwaka uliomalizika.

Anasema katika robo ya nne ya mwaka 2024, kamati ikabaini mazingira ya uchumi duniani yameimarika kwa kiwango kikubwa, kasi ya ukuaji uchumi kuongezeka, mfumuko wa bei ukaendelea kupungua katika nchi nyingi, huku mazingira ya upatikanaji fedha kwa riba nafuu katika masoko yakiwa yameimarika.

Anasema, mazingira mazuri ya kiuchumi yanatarajiwa kuendelea katika robo ya kwanza ya mwaka huu, kutokana na kuongezeko mahitaji ya walaji.

Mengine anayataja katika hilo, ni kuwapo sera wezeshi za bajeti na kuimarika mazingira ya upatikanaji



Gavana BOT, Emanuel Tutuba. **PICHA: MAKTABA**

fedha kwa riba nafuu.

Anatahadharisha kwamba, ni mambo yanayoweza kuathiriwa na migogoro ya kisiasa duniani na mivutano ya kibiashara kuongezeka.

"Uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar umeendelea kuwa imara kwa mwaka 2024. Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 5.4 katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024.

"Unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.6 katika robo ya tatu na asilimia 5.7 katika robo ya nne ya mwaka 2024, kwa kuzingatia mwenendo huo, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuwa sawia na matokeo ya ukuaji wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2024." anasema.

Pia, anataja hali ya ukuaji huu umechangiwa zaidi na ongezeko la shughuli za kilimo, usafirishaji, ujenzi, na biashara," anasema Tutuba

**SURA NZIMA MUUNGANO**

Kwa upande wa Zanzibar, anataja uchumi anakua kwa asilimia 6.8 katika robo ya kwanza na asilimia 7.2 katika robo ya pili ya mwaka 2024, makadirio yajayo ni kwamba, utakua kwa viwango hivyo kwa robo mbili zinazofuata, hivyo kufikia wastani wa ukuaji asilimia 7.2 kwa mwaka ulioisha 2024.

Anazitaja shughuli zilizochangia kukua kwake kuwa ni pamoja na utalii, ujenzi na viwanda.

Kwa mujibu wa Tutuba, ukuaji wa uchumi kwa Tanzania Bara na Zanzibar, unatarajiwa kuendelea kuwa wa kasi ya kuridhisha, kwa takriban asilimia sita na asilimia 6.8.

"Ukuaji huu unatarajiwa kuchangiwa na ongezeko la uzalishaji katika shughuli za kilimo, utekelezaji wa miradi ya ujenzi, maboresho katika usafirishaji na ugavi, nishati ya uhakika, pamoja na utekelezaji wa sera za fedha na kibajeti.

"Ukuaji wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa wa kasi ya kuridhisha mwaka 2024, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 12.5 na asilimia 16.9, mtawalia' anafafanua Tutuba

Eneo lingine analitaja Tutuba ni katika ukwasi wa fedha za kigeni, ulioongezeka kwa kiwango kikubwa katika robo ya nne ya mwaka 2024.

Anaitaja kuwa ni hali iliyotokana na kuimarika mazingira ya upatikanaji fedha duniani kutokana na kupungua kwa riba katika nchi zinazoendelea na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni nchini.

Tutuba anataja ni kutokana na shughuli za utalii, mauzo ya dhahabu, korosho na tumbaku.

Anasema thamani ya shilingi inatarajiwa kuimarika katika robo ya kwanza ya mwaka uliopo, kutokana na kuwapo ukwasi wa kutosha wa fedha za kigeni uliopatikana katika robo ya nne ya mwaka 2024,.

Hapo ana ufafanuzi wa utekelezaji wa sera ya fedha, uamuzi wa kubakiza Riba ya Benki Kuu kuwa asilimia sita, na bei za bidhaa katika soko la dunia kuwa nafuu.

Ni uamuzi anaoutaja utachangiwa na Benki Kuu kuendelea kusimamia utekelezaji wa kifungu cha sheria yake, kinachohimiza matumizi ya shilingi, unaofanya miamala ndani ya nchi kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni yasiyokuwa ya lazima.

Aidha, anasema Benki Kuu inatarajia kuendelea kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, na kuongeza pale zitakapohitajika.

Gavana anaeleza akiba iliyopo sasa ni zaidi ya Dola za Marekani bilioni 5.5 ni kiwango kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi minne.

Kuhusu mikopo kwa sekta binafsi, anasema: "Ukuaji wa fedha na mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa wa kasi ya kuridhisha mwaka 2024, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 12.5 na asilimia 16.9, mtawalia.

"Katika robo ya nne ya mwaka 2024, ujazi wa fedha ulikua kwa wastani wa asilimia 14.8 kwa mwaka ikilinganishwa na asilimia 13.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, huku mikopo kwa sekta binafsi ikikua kwa wastani wa asilimia 16.8 ikilinganishwa na asilimia 17.8.

"Mwenendo huu unatokana na ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kufuatia kuimarika kwa uchumi wa dunia na hapa nchini, pamoja na kupungua kwa vihatarishi katika ukopeshaji kufuatia kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu kufikia asilimia 3.6 mwezi Novemba 2024 kutoka asilimia 4.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2023" anasema Tutuba

Tutuba anafafanua kuwa nakisi ya urari wa malipo ya nje ilipungua kufikia asilimia 2.7 ya Pato la Taifa, ikiwa ni nakisi ya chini kabisa katika kipindi cha miaka minne iliyopita, na ikilingashwa na asilimia 3.7 mwaka 2023.

Anasema hali hiyo, ilitokana na ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yanayo kadiriwa kufikia takriban asilimia 20 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 18 katika mwaka uliotangulia, kutokana na ongezeko la shughuli za utalii, mauzo ya dhahabu, korosho na tumbaku nje ya nchi.


Uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje ya nchi ulikuwa asilimia 21 ya Pato la Taifa ukilinganisha na asilimia 20.3 mwaka 2023.

Anasema katika robo ya nne ya mwaka 2024, urari wa malipo ya kawaida ulikadiriwa kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 643.4, ikiwa ni takriban nusu ya nakisi iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

Tutuba, anasema akiba hiyo inatarajiwa kubaki katika kiwango hicho katika robo ya kwanza ya mwaka 2025 kutokana na juhudi zinazofanywa na Benki kuu katika kuongeza akiba ya fedha za kigeni, ikiwamo kununua dhahabu hapa nchini.

Hata hivyo katika mazungumzo yake, anasema Kamati itakutana tena wiki ya kwanza ya mwezi Aprili kwa ajili ya kutathmini mwenendo wa uchumi na kuamua Riba ya Benki Kuu itakayotumika katika robo ya pili ya mwaka (Aprili hadi Juni) 2025.





BANK OF TANZANIA

INDICATIVE EXCHANGE RATES

14-01-2025

| CURRENCY | | BUYING | SELLING |
|---|---|---|---|
| USA | USD | 2441.7129 | 2466.13 |
| United Kingdom | GBP | 2959.8443 | 2990.4292 |
| Euro | EUR | 2491.0355 | 2516.1924 |
| China | CNY | 333.0259 | 336.3516 |
| Japan | JPY | 15.5573 | 15.7088 |
| South Africa | ZAR | 127.6459 | 128.8954 |
| Kenya | KES | 18.8914 | 19.0068 |
| Rwanda | RWF | 1.7441 | 1.7967 |
| Uganda | UGX | 0.6346 | 0.6658 |
| Burundi | BIF | 0.8288 | 0.822 |
| | GOLD | 6517224.659 | 6583629.9706 |

NOTE: Gold price is per 1 Troy ounce
*Bei ya dhahabu ni kwa kila Wakia 1*

www.bot.go.tz @bankoftanzania

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tunaua utalii wetu, kugeuza wanyamapori matahira!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008 barua pepe:kulangwasos@gmail.com

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), huko nyuma liliwahi kuwa na Meneja Uhusiano wake mahiri, akiitwa James Lembeli, ambaye baada ya utumishi wake serikalini kukoma, aliingia kwenye siasa na kuwa Mbunge wa Kahama.

Akiwa Tanapa, aliitendea haki nafasi yake, kutokana na jinsi alivyoelimisha umma kuhusu hifadhi ya maliasili, akishirikiana vema na vyombo vya habari na akiwa tayari wakati wote kutolea ufafanuzi kwa lililotakiwa.

Wakati wake, Lembeli alijiwekea utaratibu wa kuhakikisha wanahabari nchini wanaielewa vema sekta ya maliasili na utalii, akiwapangia ratiba za kutembelea hifadhi na mbuga za wanyama zilizoko nchini.

Wanahabari walipewa fursa hizo bila gharama, wakifanya utalii wa mafunzo katika maeneo hayo kwa makundi, kwani isingewezekana kuwapeleka wote kwa pamoja, ingawa hata hivyo idadi ya wanahabari haikuwa imefumuka kama ilivyo sasa.

Alifanya hivyo, akijua wazi kuwa wananchi wote wasingeweza kupata fursa ya kutembelea hifadhi na mbuga hizo, ila walipata ya kusoma, kusikiliza na kutazama kwenye vyombo vya habari na kuelimika.

Ni bahati mbaya, kuwa Watanzania wengi hawakuwa wakijua umuhimu wa kufanya utalii wa ndani, wakiamini kazi ya kuzuru mbuga na hifadhi ni ya wageni waliofika nchini na kulipa fedha za kigeni na kuchangia Pato la Taifa.

Hivi sasa, karibu asilimia kubwa ya Watanzania wanajua umuhimu wa utalii wa ndani, ambao idadi kubwa wanaenda kujionea wanyama kwenye hifadhi na mbuga zetu, tofauti na zamani ambako walijua dhima yao ni kuwinda na kukausha vimoro.

Hiyo fursa kwa kweli haikunipita, niliipata na kuitumia vema, Lembeli aliponipangia, mimi na mpiga picha wangu, Mpoki Bukuku (Allah aendelee kumpa pumziko la milele), kuzuru hifadhi za Katavi,Rukwa; Ruaha, Iringa na Udzungwa, Morogoro na kujionea, kujifunza na kufunza pia.

Katika maeneo yote hayo, wahifadhi walikuwa wakituelezea jinsi wanyamapori wanavyotakiwa kuishi tofauti na wafugwao, nini chakula chao na maisha yao kwa ujumla, huku wakihadharisha kutupa taka dhidi ya katika hifadhi.

Wakatuambia kuwa wanyama hao hawatakiwi kula chakula kingine zaidi ya kinachopatikana porini na ndiyo sababu hairuhusiwi kuotesha chochote hifadhini au mbugani. Yaani hairuhusiwi mimea wakimbizi au wahamiaji haramu katika hifadhi hizo.

Wakisema ndiyo sababu hata magari yapitayo kwenye mbuga au hifadhi, mathalan barabara zipitazo Mikumi, Serengeti au Ngorongoro, hakuna mtu anaruhusiwa kutupa ganda la ndizi likaliwa na wanyama hao, sembuse karatasi na taka zingine.

Nia yake ni kuhakikisha kuwa uasili wa maeneo waishimo wanyama hao, unabaki palepale, kwani hata mti uliokatika kwa kuangushwa na tembo au uzee na dhoruba zingine, haukuondolewa humo bali ulisalia kuwa makazi ya wanyama wadogo na wadudu.

Pia, gogo lilisalia kama chakula chao, hivyo hakuna kigeni kilichoingizwa humo au kienyeji kilichotolewa kwa sababu yoyote ile, ili kulinda uasili wa eneo husika.

Enzi hizo, hakuna aliyeruhusiwa kuwinda au kuingiza mnyama asiye wa pori na kufanya hivyo kuliendana na adhabu kali na bila shaka inaendelea kudumu.

Lakini cha msingi, ilikuwa ni wanyamapori wabaki porini kwa utalii. Sijui ni nini kinatokea hivi sasa, tunaposhuhudia wanyamapori kwa kiasi kikubwa wakigeuzwa wa kufugwa mazizini katika maeneo kadhaa nchini, watu wakienda kuwaona na si kutalii, bali kuwalisha kwa kutumia visonzo.

Haishangazi tena, mnyama aliyeogopwa porini mpaka kuitwa mfalme wa pori au nyika, simba, anashikwa mkia, anakumbatiwa na binadamu na kutembea naye kama mwanasesere au tahira fulani hivi.

Najiuliza hivi dhana ya utalii itaendelea kushika hatamu kwa aina hii ya matendo?

Tunaamini siku zijazo watalii watakuja nchini kutazama wanyama wanaolishwa kwa visonzo kama si kunyweshwa sharubati? Kama tumeamua kuacha haya yaendelee, kuna sababu gani ya kuzuia watu kukamata wanyama pori na kuwachinja kwa kitoweo?

Kigugumizi kimetoka wapi basi cha kufungua maduka ya nyama ya porini kama Serikali siku kadhaa zilizopita, ilivyoamua na baadhi kufunguliwa na ghafla kufungwa?

Tukae chini tutafakari tena kama utalii utaendelea katika muktadha kama huu. Niko palee!



Mzigo wa dawa za kulevya ulivyonaswa hivi karibuni.



Aretas Lyimo; Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini

# Simulizi undani wa biashara dawa kulevya unavyochafua sekta nchini

**INATOKA UK.11**

toka Pakistani katika Bahari ya Hindi, zikiwa zimefichwa ndani ya jahazi lenye usajili wa nchi hiyo, ikidaiwa kufanya biashara hiyo kwa miaka 28.

Ni vilevile, kukahusishwa kilo 224.9 zilizokamatwa katika fukwe za bahari ya Hindi mkoani Dar es Salaam.

Ripoti nyingine ya mwaka 2023, inaonesha idadi ya waraibu katika mkoa wa Pwani walipatiwa tiba katika vitengo vya afya ya akili ilikuwa 62,314.

Hata hivyo, mkoa huo unatajwa kuwa wa pili, kwa kutumia dawa hizo ukiongozwa na Dar es Salaam, ambao ripoti ilionesha kuwapo waraibu 234,317.

Biashara za dawa za kulevya, zinatajwa kuwa na athari kubwa kiusalama kwa mataifa na wananchi wake.

Ni athari zinatajwa, zinawezekana kuangaliwa katika nyanja za uhalifu, usalama mipaka, kijamii, na hata siasa.

Mpango wa Kimataifa Dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa Ulioandaliwa katika ripoti ya mwaka 2020, umeonesha kuwa biashara ya dawa za kulevya huchochea ongezeko la uhalifu wa kimataifa na ndani.

Aidha, magenge ya wahalifu yanajwa hutumia silaha, kutoa rushwa, na hata kuua, ili kulinda mitandao yao.

Ripoti inafafanua kuwa, katika baadhi ya nchi za Kiafrika, mauaji ya kushukiwa kuwa wahalifu wa dawa za kulevya yameripotiwa mara nyingi.

Aidha, wizi, ujambazi, na ukatili nao unatajwa kuongezeka katika maeneo yenye kiwango kikubwa cha matumizi ya dawa za kulevya.

Kuna usalama, kudhoofika kunakotajwa kuumiza mifumo iliyoko, huku ikichangiwa na kuwapo mapato makubwa yanayotokana na biashara ya dawa za kulevya, ili kuwapa nguvu wahalifu kununua ushawishi katika taasisi za kiserikali.

Hali hiyo inatajwa kusababisha udhaifu wa mifumo ya kiusalama, katika kupambana na uhalifu huu.

Ripoti ya UNODC,2019 inaeleza wazi katika nchi kama Guinea-Bissau, ambayo imekuwa ikiitwa "dola ya dawa za kulevya" kutokana na ushawishi mkubwa wa magenge yake kwenye serikali.

Ripoti ya WHO inasema matumizi ya dawa za kulevya, yanaathiri familia, vijana, na jamii kwa ujumla.

Vilevile, suala la kuwapo ongezeko la utegemezi wa dawa za kulevya, kunasababisha kuongezeka atatizo ya kiafya, vifo na kuzorota maadili ya kijamii.

Inaelezwa, katika maeneo yenye kiwango kikubwa cha matumizi ya dawa za kulevya, vijana hukosa dira ya maisha, wakijihusisha na uhalifu au wahanga wa unyanyasaji.

Shirika liitwalo Transparency International, mwaka 2020, likasema biashara ya dawa za kulevya, inachangia kudhoofisha uchumi wa nchi na utulivu wa kisiasa.

Inafafanua kuwa, pesa zinazotokana na biashara hiyo, mara nyingi hazitumiki kwa maendeleo ya kijamii bali kwa kufadhili shughuli za uhalifu au kuficha mali haramu. Pia imekuwa chanzo cha migogoro ya kisiasa, hasa pale magenge ya wahalifu yanapopata ushawishi wa moja kwa moja katika maamuzi ya kisiasa.

Ripoti ya UNODC (2019), inaeleza kuwa nchi ya Guinea-Bissau imekuwa mfano hai wa nchi inayokumbwa na athari za biashara ya dawa za kulevya. Nchi hii ndogo ya Afrika Magharibi inatajwa kuwa kitovu cha usafirishaji wa kokaini kutoka Amerika Kusini kwenda Ulaya.

Ripoti imeeleza kuwa,Udhaifu wa serikali na ufisadi umeifanya nchi hiyo kushindwa kupambana na magenge ya dawa za kulevya, hali ambayo imeathiri sana maendeleo yake ya kiuchumi na kijamii.

Nayo asasi ya Global Initiative, 2020 katika ripoti yake imeeleza kuwa,Afrika Kusini inakabiliwa na tatizo kubwa la usambazaji na matumizi ya methamphetamine, maarufu kama "tik."

Miji kama Cape Town imeathirika vibaya, huku magenge ya wahalifu yakitawala mitaa na kushiriki katika biashara hii haramu.

UNODC,2021 imeeleza katika ripoti kuwa, Kenya na Tanzania zimeathiriwa na biashara ya heroini. Katika maeneo ya Pwani ya Kenya, miji kama Mombasa na Malindi imeripoti viwango vya juu vya matumizi ya heroini, hali inayosababisha madhara ya kiafya na kijamii.

Tanzania pia inakabiliwa na changamoto za udhibiti wa bandari zake, ambazo zimekuwa njia kuu za usafirishaji wa dawa hizi

Kamishna Lyimo anasema kumekuwepo na vipenyo zaidi ya 600 katika mwambao wa bahari ya Hindi hapa nchini na katika maziwa, hata hivyo serikali imenunua boti maalum kwa ajili ya doria katika ziwa Victoria na kuendeleza mashirikiano na mamlaka nyinginezo pamoja na jamii katika udhibiti na utoaji wa taarifa fiche.

Taarifa ya udhibiti ya mwaka 2024(DCEA)iliyotolewa na Kamishna Lyimo, inaonesha kasi ya udhibiti wa dawa za kulevya Tanzania inapanda ukilinganisha na miaka ya nyuma .Mwaka 2024 mamlaka hiyo ilikamata kilogramu 2.33 ya dawa za kulevya ukilinganisha na mwaka 2023 ambapo ukamataji ulikuwa kilogramu 1.9.



Sehemu ya dawa za kulevya za mimea

# Ridhiwani aagiza wakurugenzi kulipa madeni

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete amewaagiza wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa kulipa malimbikizo ya fedha za likizo kwa watumishi ambao wengine hawajalipwa tangu mwaka 2018.

Aidha, ameahidi kukaa na mawaziri wa kisekta ili kutafutia ufumbuzi wa hoja nane zilizotolewa na Chama Cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) ikiwamo suala la watumishi wa kada za afya kulipia leseni zao kila mwaka.

Akifungua kikao cha baraza kuu la chama hicho jijini hapa, Kikwete alisema serikali imesikia hoja hizo na kuagiza wakurugenzi hao wasimamie ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri zao ili kutengeneza uwezo wa kulipa malimbikizo ya mishahara na likizo kwa watumishi.

"Likizo ni haki ya mtumishi na ipo kwa mujibu wa sheria na serikali inatambua kuna halmashauri ambazo zina vyanzo vidogo vya mapato na pamoja na jitihada za serikali za kuzipatia ruzuku lakini bado kuna maeneo yanahitaji msisitizo, pamoja na kulichukua jambo hili kutafuta ufumbuzi wa kudumu niwatake waajiri wote walipe likizo kwa wakati," alisema.

**Kazi nyingine zitakazofanyika ni kufungua viwanda vya kuzalisha mvinyo wa asali, kujenga hoteli na viwanja vya mpira ili timu kubwa...**

Kadhalika, aliagiza wakurugenzi hao kulipa posho za madaraka kwa watumishi wa kada hasa za maofisa watendaji wa kata kutokana na kudaiwa hawajalipwa kwa miezi nane.

Pamoja na hayo, alielekeza waajiri wote nchini kuhakikisha wanahuwisha mabaraza ya wafanyakazi na kusisitiza kuwa serikali haitamfumbia macho mwajiri yoyote ambaye hataki kutimizwa takwa la kisheria.

Akizungumzia kuhusu watumishi wa umma wanaodhalilishwa, Ridhiwan alikemea tabia ya waajiri kuwatangaza kwenye vyombo vya habari na kutaja sababu za kuwafukuza kwa kuwa hali hiyo inawanyima haki zingine.

Alisema serikali imeendelea kuzingatia maslahi ya wafanyakazi kwa kuongeza kikokotoo ambacho kwa sasa kimefikia asilimia 40 na kinalipwa vizuri.

Mwenyekiti wa TALGWU Taifa ambaye pia ni Rais wa Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamhokya alipongeza serikali kwa kuendelea kutatua kero zinazowakabili watumishi wa umma.

Alisema serikali imesikia kilio cha muda mrefu cha watumishi waliokuwa wanalipwa mishahara kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na kwasasa wanalipwa kupitia mfuko mkuu wa serikali, sambamba na kupandisha madaraja na kulipa madai yao.

Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima alitaja hoja hizo nane kuwa ni kutolipwa kwa wakati fedha za uhamisho, likizo, posho ya madaraka, kutotekeleza kikamilifu kwa mfumo wa upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma (PEPMIS).

Zingine ni changamoto ya miundo ya utumishi na upandishaji wa vyeo, kutohuwisha mabaraza ya wafanyakazi na kuchelewa kwa mashauri ya kikazi katika Tume ya Utumishi wa Umma.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akiangalia moja ya mahindi yaliyozalishwa katika shamba darasa la Jeshi la Magereza, alipofanya ziara katika Makao Makuu ya jeshi hilo, Msalato mkoani humo jana, kulia kwake ni Mkuu wa Jeshi hilo, Kamishna Jenerali Jeremiah Katungu. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mwigulu ataja sababu miradi kukwama

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Fedha, Dk.Mwigulu Nchemba, ametaja sababu za kusimama kwa baadhi ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa nchini ikiwamo ya barabara kwamba ni kutokana na serikali kuelekeza fedha nyingi kwenye miradi mikubwa ya kimkakati ili ikamilike kwa uharaka.

Akizungumza juzi kwenye kikao cha 48 cha bodi ya barabara mkoani Singida, alisema serikali iliamua kuelekeza fedha nyingi kwenye miradi ya kimkakakati ili iweze kukamilika kwanza kwasababu baadhi ilikuwa katika hatua za mwisho.

Dk. Mwigulu alitaja miradi hiyo iliyopewa kipaumbele kukamilishwa kuwa ni ujenzi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) ambalo kwa mwezi mmoja serikali ilikuwa ikipeleka zaidi ya Sh.bilioni 400.

Dk.Mwigulu alisema hatua ya serikali kufunga mkanda imesaidia kukamilisha mradi wa ujenzi wa Bwala la Kufua Umeme la Julius Nyerere ambalo sasa umeme unazalishwa.

Alitaja miradi mingine ambayo serikali iliamua kuipa kipaumbele kwanza ni mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na ujenzi wa Daraja la Magufuli la Kigongo-Busisi.

Aliongeza kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 21, 2024 nalo pia lilipewa kipaumbele kwanza ambapo serikali ilijitegemea kwa kugharamia uchaguzi huo kwa fedha zake bila kutegemea wafadhili.

Alisema baada ya kukamilika kwa miradi hiyo ya kimkakati sasa fedha zimeanza kutiririka kupelekwa kwenye miradi ambayo ilikuwa imesimama.

Dk.Mwigulu alisema katika suala la ujenzi wa barabara serikali ina mpango kuruhusu fedha za makusanyo yanayofanywa na TANROADS na TARURA zinapokuwa zinatosheleza zitumike kujenga barabara mpya.

# Ulega azuru kipande korofi cha barabara, atoa agizo

**Na Renatha Msungu** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega amezuru kipande korofi cha barabara Kuu ya Mtanana kutoka Morogoro hadi Dodoma na kuagiza ujenzi wa daraja kuharakishwa kabla ya mvua za masika kuanza kunyesha ili kukabiliana na mafuriko.

Ujenzi wa kipande hicho chenye urefu wa kilomita sita, unatarajia kukamilika Juni, mwaka huu.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo hilo, Ulega, alisema kukamilika kwa daraja hilo kutasaidia kuondoa changamoto ya muda mrefu kwa wananchi wa eneo hilo ya kukosa usafiri.

Alimtaka mkandarasi kufanya ukarabati katika sehemu ambazo zimeharibika na kukamilisha kabla ya mvua hizo za masika kuanza kunyesha ili kuepuka mafuriko

Ulega alisema eneo hilo linasababisha changamoto kubwa mvua kubwa zinaponyesha kutokana na kujaa maji na kusababisha msongamano wa magari kutoka Dodoma kwenda Morogoro na maeneo mengine na kuwa kero kwa wananchi.

"Daraja hili linatakiwa kukamilika kabla ya mvua za masika kuanza kunyesha, mkandarasi unapaswa kuongeza kasi ya ujenzi wa daraja hilo ili kuepuka madhara yatokanayo na mvua," alisema.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo wa dharula katika bonde hilo la mafuriko la Mtanana Italia ni mwarobaini wa kuondoa athari za vifo na ajali zinazosababishwa na mafuriko kipindi cha mvua.

Meneja wa Wakala wa Barbara Nchini (TANROADS) Mkoa wa Dodoma, Zuhura Amani, alisema ujenzi huo umegharimu zaidi ya sh bilioni 26 na kwamba umefikia asilimia 49.8.

Zuhura, alisema mkandarasi anaendelea vizuri na ujenzi ili kuhakikisha ujenzi wa daraja hilo unakamilika kwa muda uliopangwa na serikali kabla ya mvua hizo kuanza kunyesha.

"Tunaamini mkandarasi atakamilisha ndani ya muda uliopangwa kuepusha madhara katika eneo hilo kipindi cha mvua," alisema.

Omary Rajabu, Mkazi wa Mtanana, aliishkuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo na kuwaondelea changamoto ya eneo hilo kukumbwa na mafuriko na kukwamisha shughuli zao kwa kukosa usafiri.

Rajabu, alisema wananchi wamekuwa wakipata tabu kwa kukosa usafiri na wengine kufa kwa kusombwa na mafuriko wakati mvua za masika zinaponyesha.



# Vifaa vya bil 3/- kutumika kuzalisha umeme wa joto ardhi Ziwa Ngosi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imenunua vifaa vya Sh. bilioni tatu kwa ajili ya kuchoronga visima vya kuzalishia umeme wa joto ardhi katika eneo la Ziwa Ngosi katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya. Vifaa hivyo ambavyo vimenunuliwa kutoka katika mataifa mbalimbali, viliwasili jijini Mbeya juzi na kupokelewa na maofisa wa Kampuni ya Uendelezaji wa Joto Ardhi nchini (TGDC) ambayo ndiyo inatekeleza miradi hiyo.

Akizungumza wakati wa mapokezi ya vifaa hivyo, Mkurugenzi wa TGDC, Mhandisi Shakiru Kajugusi alisema baada ya kupokea vifaa hivyo wamevikagua na kujiridhisha kuwa viko katika hali nzuri na hivyo wanakusudia kuanza kuvipeleka kwenye eneo la mradi.

Alisema mradi wa Ziwa Ngosi ni miongoni mwa miradi ya kipaumbele na hivyo watahakikisha wanasimamia ili vifaa vifike mapema na kuanza utekelezaji wa mradi.

"Tunatarajiwa kwamba mwishoni Februari ama mwanzoni mwa Machi tuwe tumeanza utekelezaji wa mradi huu na kwa sasa kwa kuwa vifaa vimefika hatutakuwa na sababu ya kukwama tena," alisema Kajugusi.

> **"Tunatarajiwa kwamba mwishoni Februari ama mwanzoni mwa Machi tuwe tumeanza utekelezaji wa mradi huu na kwa sasa kwa kuwa vifaa vimefika hatutakuwa na sababu..."**

Kaimu Meneja wa Mradi wa Joto Ardhi wa Ziwa Ngozi, Mhandisi Hoja Honori aliwataka wananchi wanaozunguka mradi huo kushiriki katika ulinzi na usalama wa vifaa hivyo ili visihujumiwe na kuharibu utekelezaji wa mradi.

Alisema vifaa hivyo vimegharimu fedha nyingi na hivyo ni lazima vilindwe ili kuhakikisha vinafanya kazi iliyokusudiwa na serikali hasa kuzalisha umeme.

Alisema mradi huo ukikamilika utakuwa na faida kwa taifa hasa kuongeza kiwango cha umeme ambao utachangia kwenye shughuli zingine za maendeleo.

"Serikali ilitoa fedha nyingi sana kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivi, sasa ni wajibu wa jamii ya watu wanaozunguka mradi wetu kusaidiana nasi kulinda mradi vifaa hivi, mradi ukikamilika hata wao watanufaika kwa kiwango kikubwa," alisema Honori. Fundi uchorongaji wa visima hivyo, Safina Yunde alisema ili kuimarisha ujirani mwema na wananchi wa vijiji vinavyozunguka eneo la mradi wanakusudia kuwaajiri wananchi hao kwenye shughuli mbalimbali ambazo hazihitaji utaalamu.

Alisema baadhi ya kazi ambazo wanawaajiri wananchi hao ni pamoja na ulinzi, kubeba vifaa na shughuli zingine ndogo ndogo ambazo zinaweza kufanywa na wananchi kwa kusimamiwa na wataalamu.

Kampuni ya TGDC imeshachoronga kisima cha mfano katika eneo la Mbaka - Kyejo katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe na sasa mradi mkubwa wa Ziwa Ngosi.




Wabeba mizigo wa Stendi Kuu ya Mabasi ya Mikoani ya Magufuli, wakiwa wamekaa juu ya matoroli yao, wakisubiri abiria katika kituo cha daladala Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana, ili wapate ujira wa siku. **PICHA: SABATO KASIKA**

## RC atoa siku 10 ujenzi shule ya sekondari ukamilike

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya, Mbaraka Alhaj Batenga ametoa siku 10 kwa mkandarasi na kamati ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Nkung'ungu kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na miundombinu ya shule hiyo ili wanafunzi wa kidato cha kwanza waliochaguliwa waanze masomo.

Batenga alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika tarafa ya Kipembawe iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

"Natoa siku 10 na sitoongeza hata siku moja kwa mkandarasi na kamati ya ujenzi kukamilisha ujenzi wa Shule ya Sekondari Nkung'ungu, nataka muongeze muda wa kufanya kazi ili wanafunzi waanze masomo" amesema. Pia alimtaka mzabuni wa mradi wa ujenzi wa shule hiyo kurudisha fedha za usafirishaji wa vifaa vya ujenzi kutokana na kukiuka mkataba kwa kununua vifaa na kushindwa kufifikisha kwenye eneo la mradi huo.

Alimtaka mhandisi wa halmashauri hiyo kusimamia mradi huo ili kuhakikisha unajengwa kwa viwango vinavyotakiwa na kuhakikisha thamani halisi ya fedha inaonekana na kwamba endapo watakiuka hatua zitachukuliwa. Mwenyekiti wa Kamati wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari Nkung'ungu, Mwalimu Erasto Kilasi aliahidi kuwasimamia kikamilifu wasambazaji wa vifaa vya ujenzi na mafundi ujenzi kuharakisha ujenzi wa shule unakamilika.

# Waomba kutatuliwa migogoro kuepuka mauaji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BAADA ya kuibuka mapigano baina ya wakulima wilayani Mbarali mkoani Mbeya na kusababisha vifo vya watu wawili na kujeruhi wengine wanane, wananchi wa Kata za Igurusi na Itamboleo, wameomba serikali kushughulikia migogoro inayoendelea kwenye maeneo yao ili kuepusha madhara.

Wananchi hao walisema kuna migogoro mingine inaendelea kufukuta katika maeneo ikiwemo ya wakulima na wafugaji ambayo inaweza kusababisha mapigano na hivyo wakaomba serikali iwasaidie kutatua.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya,iliyokuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Mbarali.

Mmoja wa wananchi hao, Hussein Yusuph alisema katika kipindi hiki ambacho wanaendelea na maandalizi ya kilimo kuna migogoro ambayo inafukuta baina yao na wafugaji.

Alisema wakulima wanaandaa mashamba na kumwaga mbegu za mpunga lakini wafugaji wanachunga mifugo yao hali ambayo inahatarisha usalama.

Alisema wamekuwa wakitoa taarifa mara kwa mara kwenye vituo vya polisi lakini wanapatiwa majibu ambayo yanahatarisha zaidi hali ya amani na usalama wao.

"Tunakwenda polisi wanatuambia tuzipige picha hizo ng'ombe kama ushahidi, sasa sisi tunaogopa kwa sababu wale wafugaji wakikuona unapiga picha mifugo yao unakuwa umekwisha, tunaomba sana serikali itusaidie hawa watu wasichungie mifugo kwenye mashamba yetu," alisema Yusuph.

Naye Halifa Mahenge alisema kwa sasa wenzao wa Luhanga wameshaanza kuuana hali ambayo inaweza ikawafikia na wao katika eneo lao.

Alisema tatizo hilo linasababishwa na serikali kuwaondoa baadhi yao kwenye maeneo ambayo yalikuwa ya asili na hivyo kulazimika kujikusanya kwenye maeneo machache.

Frank Mkwawa alisema kuna eneo la shamba la mifugo ambalo lilitakiwa litumiwe na wafugaji lakini halitumiki kwa shughuli hiyo na badala yake kuna watu wachache wamejimilikisha wanalima na hivyo kusababisha shughuli za kilimo na mifugo kuingiliana.

Hivyo, aliomba serikali kuwaondoa wakulima wanaolima kwenye shamba hilo la NARCO ili litumike kwa shughuli za ufugaji na maeneo ya mashamba yabaki kwa ajili ya kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliliagiza Jeshi la Polisi kuimarisha doria kwenye maeneo yenye migogoro na kuwakamata kisha kuwachukulia hatua za kisheria wanao husika na kuvunja amani maeneo ya kilimo.

Pia, aliwataka viongozi wa vijiji kushiriki katika kudhibiti migogoro kwa kuhakikisha kila shughuli inafanyika kwenye eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya shughuli husika.



# Serikali yaanza mapambano dhidi ya lishe duni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla amesema serikali imeanza kuchukua hatua katika kuimarisha huduma za lishe na afya bora kwa wananchi.

Aliyasema hayo juzi katika hafla ya uzinduzi wa mpango mkakati wa kisekta wa lishe Zanzibar 2025-2029 uliofanyika visiwani hapa.

Alisema serikali inatambua kuwa lishe bora ndiyo msingi imara wa maisha ya mwanadamu na ndiyo tegemeo lenye kutoa vijana wenye weledi na nguvu kazi ya kujenga taifa lenye maendeleo endelevu.

Alisema lengo la mpango mkakati huo ni kuimarisha afya za wananchi na kuondoa changamoto zinazosababishwa na ukosefu wa lishe bora ikiwemo udumavu wa watoto, uzito pungufu na utapiamlo hususani kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano na wanawake wenye umri wa kujifungua ambao ndiyo walengwa wakubwa wa mpango huo.

Hemed alisema mpango mkakati wa lishe utakuwa ni chachu ya utekelezaji wa mipango mingine kisekta na mikakati mbalimbali ya serikali inayolenga kuboresha lishe na kuimarisha afya ya jamii.

**Alisema pia italenga kupunguza maradhi pamoja na kuipunguzia serikali mzigo mkubwa wa kugharamia matibabu kwa wagonjwa wa ndani na wale wanaosafirishwa nje ya nchi.**

Alisema pia italenga kupunguza maradhi pamoja na kuipunguzia serikali mzigo mkubwa wa kugharamia matibabu kwa wagonjwa wa ndani na wale wanaosafirishwa nje ya nchi.

Hivyo, aliwataka viongozi wa sekta zote husika ambazo zimetajwa katika mkakati huo kufanya wajibu wao ili kuendana na kasi ya serikali katika kuimarisha afya za wananchi.

Pia, aliitaka jamii kufuata utaratibu mzuri wa lishe bora ili kuondokana na changamoto za kiafya zinazoweza kuepukika.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazurui, alisema ili kuimarisha afya ya mama na mtoto wizara imejipanga kuboresha viashiria vya lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wajawazito na wanafunzi kwa lengo la kutengeneza jamii yenye afya na lishe bora kwa maendeleo ya taifa.

Mazurui alisema Wizara ya Afya imeanzisha programu za lishe katika ngazi ya mkoa na shuleni ili kutanua zaidi uwelewa kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwa na lishe bora ili kujenga jamii imara na yenye lishe endelevu

Mkurugenzi Mkaazi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF) Tanzania, Elke Wisch, alisema ukuaji mzuri wa mtoto unategemea upatikanaji wa lishe bora.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa asilimia 70 ya watoto nchini hawakuwi vizuri kutokana na kutopatikana kwa lishe bora kwa mama na mtoto.

Alisema mpango mkakati wa kisekta wa lishe Zanzibar una lengo la kuhakikisha watoto na wajawazito wanafikiwa na huduma za afya ikiwemo lishe bora, ili kuandaa kizazi bora kisicho na changamoto ya udumavu, utapiamlo na maradhi nyemelezi kwa maslahi mapana ya Zanzibar.



Mafundi wakirekebisha miundombinu ya jengo la mikutano la Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam jana, utakapofanyika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati ya Umeme, mwezi huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wananchi wapewa tahadhari dhidi ya saratani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kuchukuwa tahadhari kutokana na ongezeko la ugonjwa wa saratani.

Ushauri huo umetolewa na Meneja Msaidizi wa Kitengo cha Maradhi Yasioambukiza (NCDs UNIT) kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Zuhura Saleh Amour.

Zuhura alitoa ushauri huo wakati wa mafunzo kwa maofisa mipango wa wizara mbalimbali za serikali, yaliyofanyika katika Kituo cha Afya ya Uzazi na Mtoto Kidongo Chekundu Wilaya ya Mjini Unguja.

Alisema Taasisi ya Saratani ya Ocean Road jijini Dar-es-Salaam inapokea wagonjwa wengi kutoka Zanzibar, hivyo ni vyema jamii kupima afya mapema ili kujua matatizo waliyonayo na kuyapatia ufumbuzi wa haraka.

"Kadri umri unavyokwenda kuna hatari ya kupata saratani na baadhi ya wenzetu kinababa wanachelewa kupima afya zao na kupelekea kukosa huduma mapema jambo ambalo linachangia ongezeko la maradhi hayo" alisema Zuhura.

Aidha, alisema iwapo maradhi ya saratani yatagundulika katika hatua za awali, yanaweza kutibika na kuokoa maisha ya mtu.

Alisema tatizo la saratani linapoanza huwa halionyeshi dalili, hivyo ni vyema jamii kuhamasika kufanya mazoezi ili kupunguza uzito na kubaki salama.

Hata hivyo alitaka jamii kupunguza matumizi ya mafuta kwa wingi ili kuzuia kuganda katika mifupa na kusababisha maradhi yasiyoambukiza.

Mkufunzi wa maradhi yasiyoambukiza kutoka Hospitali ya Mnazimmoja, Dk. Salum Saleh Mwinyi alitaka jamii kuchukuwa hatua kwa watoto na vijana wanaojishughulisha na utumiaji wa sigara, shisha, tumbaku, bangi kwasababu vinachangia kwa kiasi kikubwa kuathiri jamii.

Alisema vifo vinavyotokana na tumbaku ni vingi kuliko UKIMWI, malaria na kifua kikuu, huku akibainisha kuwa katika nchi zenye maendeleo, matumizi ya tumbaku yamepungua ikilinganishwa na nchi zisizokuwa na maendeleo.

Meneja wa Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Maradhi Yasioambukiza, Haji Khamis Fundi, alisema lengo la kuanzishwa jumuiya hiyo ni kuwasaidia wagonjwa, kuwaunganisha pamoja na kupaza sauti zao.

Alisema jumuiya hiyo inatoa utetezi, ushauri nasaha kwa waathirika wa maradhi hayo sambamba na kupima afya zao, ili kuishi katika hali ya amani na kufuata maelekezo wanayopewa na wataalamu wa afya.

# Serikali yawatoa hofu wakazi Kizimkazi, ujenzi bandari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema utekelezaji mkakati wa ujenzi wa bandari katika Kijiji Cha Kizimkazi Kusini Unguja utazingatia maslahi mapana kwa jamii.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar, Akif Ali Khamis, aliyasema hayo katika kikao cha awali cha uwasilishaji wa andiko la mradi wa ujenzi huo kwa baadhi ya wakazi wa Kizimkazi ambao maeneo yao yatachukuliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa bandari hiyo.

Alisema andiko la mradi huo pamoja na shughuli nyingine zilizopangwa kwa sasa utazingatia mambo matatu yakiwemo ya kufanya upembuzi yakinifujuu ya ujengwaji wa bandari, ulipaji wa fidia kwa waathirika wa mradi pamoja na ujengwaji wa uzio kwa eneo lote la mradi.

Hata hivyo alisema dhamira ya serikali ya kutekeleza mradi huo unalenga kuboresha miundo mbinu ya usafiri na biashara ili kuchochea kasi ya maendeleo na ukuwaji uchumi.

Aidha, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kutoa ushirikiano ili mradi huo unafanikiwa na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, aliwataka wananchi wa Kijiji cha Kizimkazi kwamba kuwa tayari kupisha ujenzi wa bandari hiyo pamoja na kutoa maoni yatakayosaidia kufanikisha vyema ujenzi huo ambao unalenga kutoa fursa za kiuchumi kwa wananchi wa Mkoa wa Kusini.

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho, walisema hawana mashaka na ujenzi wa bandari hiyo bali serikali izingatie utendaji wa haki katika ulipaji wa fidia ili waathiriwa wa zoezi hilo wanaondokana na usumbufu wakati utapowadia wa kupisha ujenzi huo.

# Mfuko nishati safi ya kupikia waja

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI inaendelea na ukamilishaji taratibu za kuanzisha Mfuko wa Nishati Safi ya Kupikia ili kuweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis aliarifu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jana jijini Dodoma alipowasilisha taarifa ya utekelezaji maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati iliyowasilishwa bungeni Februari, 2024.

Alisema Kanuni za Usimamizi wa Miradi ya Biashara ya Kaboni zimebainisha ruzuku kupitia hakimiliki za kaboni zinazopatikana kutokana na kupunguza matumizi ya nishati inayochafua mazingira, hivyo ruzuku hii ni sehemu ya juhudi za kitaifa za kutekeleza malengo ya kupunguza gharama kwa watumiaji wa nishati safi.

Khamisi alieleza kamati hiyo kuwa katika jitihada za kupunguza gharama za matumizi ya nishati mbadala, serikali imetia saini makubaliano ya awali na wawekezaji kuhusu ruzuku ya Sh. bilioni 8.64 kwenye nishati safi ya kupikia ambapo jumla ya majiko 452,455 yamepata ruzuku.

Naibu Waziri Khamis alisema serikali inaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kwa njia mbalimbali, ikiwamo utoaji elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, ziara za viongozi.

Kwa upande mwingine alisema kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea

kushirikiana na wadau wengine wakiwamo Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa lengo la kuhamasisha na kuhimiza halmashauri zote za vijiji kuainisha misitu yote ya vijiji yenye sifa ya kuingizwa katika Mpango wa Biashara ya Kaboni.

Alifafanua kuwa uhamasishaji jamii kuhusu umuhimu wa biashara ya kaboni katika kuhifadhi mazingira na kuongeza kipato kwa jamii unaendelea kutolewa kwa wananchi ambapo serikali inaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa mikataba ya biashara ya kaboni inanufaisha wananchi na inafanyika kwa mujibu wa Kanuni za usimamizi wa biashara ya kaboni.

Kwa upande wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira inayoongozwa na Mwenyekiti Jackson Kiswaga, imepongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuwakutanisha wadau na kujadili changamoto za mazingira ili kuzipatia ufumbuzi.

Pamoja na hayo imesisitiza elimu ya mazingira iendelee kutolewa ili wananchi wawe na uelewa na kuachana na vitendo vya uharibifu wa mazingira vikiwamo vya uchomaji na ukataji miti.

Pia imesema elimu ya nishati safi ipewe msukumo kwa kuwa wananchi wengi hususan wa maeneo ya vijijini hawana uelewa wa umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, hivyo kwa kuwapa elimu wataachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Cyprian Luhemeja, akifafanua hoja, alisema hadi kufikia Desemba 30, 2024, maombi ya miradi 65 ya biashara ya kaboni yalikuwa yamepokewa.

Alifafanua kuwa jumla ya miradi sita imepata barua za kukubaliwa kuanza mchakato wakati miradi sita imetimiza vigezo na hatua za kupatiwa barua inaendelea.

## JK aambatana katika SGR na wajumbe 700 mkutano CCM

Na Pilly Kigome

WAJUMBE 750 wa Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) jana walisafiri kwa kutumia treni ya kisasa kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, huku Rais mstaafu Jakaya Kikwete akiongoza msafara huo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa alisema wajumbe hao wanakwenda Dodoma kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM unaotarajiwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia kesho.

Alisema hatua ya wajumbe hao kutumia usafiri wa treni ya kisasa ni heshima kwa TRC na imewapa faraja, heshima na moyo wa kuendelea kufanya vizuri zaidi.

Kadogosa alisema kuwa msafara wa wajumbe hao ni kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar pamoja na wasanii zaidi ya 100 na waandishi wa habari.

Alisema hatua ya wajumbe hao kutumia usafiri huo watakuwa wameona namna utekelezaji Ilani ya CCM ulivyofanyika pamoja na miradi ya maendeleo ilivyotekelezwa.

Alisema hadi kufikia jana TRC kupitia treni ya kisasa, wamesafirisha watu milioni 1.4 tangu kuanza kwa usafiri huo Juni mwaka jana.

Alisema kuwa katika maandalizi ya kuanza usafiri wa mizigo, TRC imeshaleta mabehewa 264 kati ya 1,430 na majaribio yameshaanza.

"Tunajivunia sana SGR na tayari kuna baadhi ya wafanyabiashara wameshaanza kuomba kuchukulia mizigo yao Dodoma na wameshakaa mkao wa kula," alisema Kadogosa.

Alitoa onyo kwa watu wanaohujumu usafiri huo, akisema watawashughulikia kwa mujibu wa sheria pindi watakapokamatwa.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wajumbe waliosafiri na treni hiyo, Julius Kaondo alisema kutokana na mshikamano mkubwa uliopo ndani ya chama hicho, wamepata heshima kubwa ya kusafiri kwa usafiri huo.

Aliomba serikali kuwachukulia hatua stahiki wote watakaokamatwa wanahujumu usafiri huo, akisema wanarudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Mkoa wa Pwani, Zainabu Vullu alisema mkutano huo ni wa kipekee kwa sababu unakwenda kumpa kiongozi muhimu ndani ya chama.


### KUPOTEA KWA CHETI



**ZEPHANIA LUCAS GUNDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1093/0107** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ALDERSGATE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/3259/2025.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WARIOBA BUHEMBERE KANIRE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za Usajili **T. 820 DRA** aina ya **KLUGER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi: **PHO/SHI/KAH/696/2025.**

FOMU MIRATHI - 2

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 2060/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMISI BAKARI JUMA WA..............**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWATABU ABEID KISUKARI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 01 mwaka 2025 saa 4:00 asubuhi kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 27 mwezi 12 mwaka 2024.

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA MADAI YA GHARAMA NA 28289 LA MWAKA 2024**

**MILO GROUP LIMITED....................MDAI TUZO**

**DHIDI YA**

**AVM DILLINGHAM......................MDAIWA TUZO**

**KWA: AVM DILLINGHAM – POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakama binafsi au Wakili wenu tarehe 30/01/2025 siku ya Ijumaa saa 3:00 kamili asubuhi ambapo shauri limepangwa kutajwa.
**ELEWA KWAMBA** ukikosa kufika siku hiyo, shauri litapangwa kusikilizwa bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 20/12/2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

### KUPOTEA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**MAIKO MASESA NGEGESHI** msimamizi wa mirathi ya marehemu **MASESA NGEGESHI** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba **15 kitalu"Y"** kilichopo Ibinzamata Manispaa ya Shinyanga. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu Taarifa ya Polisi.**SHI/SHI/RB/417246/2022.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AUGUSTINO SHAURI MANDA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 677 DMY TOYOTA KLUGER.** Yeyote akatayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/KYE/798/2025.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mhakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**

**Shauri la TALAKA Na 02/2025**

**Jina la Mdai: CATHERINE CHARLES SHADRACK**

**Jina la Mdaiwa: KISHIWA SIMON LUBIGILI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: KISHIWA SIMON LUBIGILI**
**WA GEITA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 20 Mwezi 01 Mwaka 2025 Saa 08.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 09 Mwezi 01 Mwaka 2025

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...2/2025**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SALUMU JABIRI MSAMBWE wa MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FATUMA SALUMU JABIRI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 23 Mwezi 1 Mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 16 mwezi 1 mwaka 2025

16 Mwezi 1 Mwaka 2025
HAKIMU

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU GWANDUMI AMOS MWAKYOMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T303BKN** aina ya **MITSUBISH FUSO.** Engine **No.6D16810112,** Chasis No. **FK617K513684** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/DOD/DOD/RB/2973/2025**

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JACOB BROWN MUSHI** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (PASSPORT) yenye namba **TAE 264764** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **JNIA/RB/12/2025.**

# Biden aonya Marekani kuongozwa na matajiri

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden ameonya kuhusu tishio la taifa hilo kuongozwa na kundi la watu wachache ambalo limejitokeza.

Katika hotuba yake ya kuaga baada ya kumaliza uongozi wake na huduma yake katika siasa, alisema utawala huo wa watu wachache matajiri unatishia demokrasia, haki na uhuru.

"Leo, utawala wa wachache umeanza kujitokeza katika Marekani wenye utajiri mkubwa, nguvu na ushawishi ambao unatishia demokrasia yetu yote, haki zetu za msingi na uhuru," alisema Rais Biden.

Kiongozi huyo anayemaliza kipindi cha urais akiwa na umri wa miaka 82, alilenga uongozi unaokuja wa Donald Trump wenye utajiri mkubwa na kusema unaweza kuwa na nguvu ya ajabu isiyodhibitiwa na kuwashinda Wamarekani.

Pia alitumia hotuba yake ya mwisho iliyopeperushwa moja kwa moja kutoka Ikulu ya White House kutoa maonyo kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na upotoshaji wa mitandao ya kijamii.

Akizungumza huku familia yake ikiwa inashuhudia, aliangazia rekodi yake ya utawala wa muhula mmoja, akisifia utengenezaji wa fursa za ajira, matumizi ya miundombinu, huduma ya afya, kuongoza nchi kutoka katika janga la corona, na kuifanya Marekani kuwa nchi salama.

"Itachukua muda kuona matokeo kamili ya yote ambayo tumefanya pamoja, lakini mbegu zimepandwa, zitakua, zitachipuza na kuchanua kwa miongo kadhaa ijayo". alisema

Biden alimtakia mafanikio Donald Trump, lakini akionya kwamba kuna mengi ambayo yako hatarini kwa sasa.

**BBC**



# Wapalestina washerehekea kusitisha mapigano Gaza

**GAZA, Palestina**

WAPALESTINA wanaoishi Ukanda wa Gaza wameingia mitaani kushangilia makubaliano ya kusitisha vita yaliyofikiwa usiku wa kuamkia jana kati ya Israel na Hamas.

Pande zote mbili zilikubaliana katika mkutano uliofanyika nchini Qatar kusitisha mapigano na kuwaachilia mateka baada ya miezi 15 ya vita.

Waziri Mkuu wa Qatar, Shekhe Mohammed bin Abdul Rahman Al Thani, alisema makubaliano hayo yataanza kutekelezwa siku ya Jumapili mara yatakapopitishwa na baraza la mawaziri la Israel.

Rais wa Marekani Joe Biden alisema Israel itasitisha mapigano Ukanda wa Gaza, pamoja na kuongeza msaada wa kibinadamu unaohitajika kwa raia wa Palestina, na kuwaunganisha mateka na familia zao.

Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, alisema maelezo ya mwisho ya mkataba huo bado yanashughulikiwa, lakini alimshukuru Rais Biden kwa kuendeleza mchakato huo.

Kiongozi wa Hamas Khalil al-Hayya, alisema makubliano hayo ni matokeo ya ustahimilivu wa Wapalestina.

Wapalestina wengi na familia za mateka wa Israel zilisherehekea baada ya kupata taarifa hiyo.

Hata hivyo, katika uwanja wa mapambano hali ilikuwa tofauti katika maeneo ya Gaza.

Shirika la Ulinzi la Raia linaloendeshwa na Hamas liliripoti kuwa mashambulizi ya anga ya Israel yaliua zaidi ya watu 20 muda mchache baada ya tangazo hilo.

Watu waliouawa walikuwa 12 ambao walikuwa wakiishi katika kizuizi cha makazi katika kitongoji cha Sheikh Radwan kilichopo Jiji la Gaza.

Baraza la Mawaziri la Israel linatazamiwa kukutana ili kuidhinisha makubaliano hayo, huku makubaliano ya awali ya wiki sita yakitarajiwa kuanza Jumapili.

Israel ilianzisha kampeni ya kuiangamiza Hamas ambayo imechukuliwa kama kundi la kigaidi, kujibu shambulio la Oktoba 7, 2023, wakati Hamas walipovuka mpaka na kuwaua watu 1,200 na wengine 251 walichukuliwa mateka.

Katika vita hiyo zaidi ya watu 46,700 wameuawa Ukanda wa Gaza, kwa mujibu wa wizara ya afya ya eneo hilo inayoendeshwa na Hamas.

Watu milioni 2.3 wamekimbia makazi yao, huku uharibifu mkubwa ukionekana katika eneo hilo. Pia Gaza inakabiliwa na uhaba wa chakula, mafuta, dawa na makazi.

Israel inasema mateka 94 bado wanazuiliwa na Hamas, ambapo 34 kati yao wanakisiwa kufariki. Aidha, kuna Waisraeli wanne waliotekwa nyara kabla ya vita, wawili kati yao wamepoteza maisha.

Wakati huo huo, Wapalestina wanaoishi Gaza waliambia BBC Arabic kuhusu hisia zao juu ya makubaliano hayo ya kusitisha mapigano.

Mwanamke ambaye mwanawe, Nabil Mohammed Zidan Nasser, aliuawa wakati wa vita, alisema alihisi mchanganyiko wa furaha na huzuni aliposikia habari hizo.

"Asante Mungu, ninawapongeza watu wetu kwa mapatano haya, watu wa Gaza waliozingirwa na wanaohangaika, na Mungu akipenda utatekelezwa kikamilifu" alisema

Mwanaume mmoja, alitoa shukrani zake kwa nchi za Kiarabu kwa juhudi zao zilizosaidia kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano.

"Tuliogopa kwamba zamu yetu ingefika na tukafa katika vita hivi, bila kutaja mateso tuliopitia kutokana na ukosefu wa chakula na vinywaji, na kutopatikana kwa maji." Alisema. **BBC**



# Waliopoteza maisha mgodini wafikia 78

**CAPETOWN, Afrika Kusini**

JESHI la polisi nchini Afrika Kusini limetangaza kumaliza operesheni ya uokoaji wa watu waliokwama katika mgodi wa dhahabu uliotelekezwa katika eneo la Stilfotein.

Mpaka kazi ya uokoaji inakamilika juzi wachimba madini 78 wamethibitishwa kufariki, huku wengine 246 wametolewa wakiwa hai.

Makundi ya kutetea haki za binadamu nchini Afrika Kusini yalisema kuwa idadi ya vifo inaweza kuwa kubwa zaidi na kwamba waathiriwa wanashukiwa kuwa walifariki kwa njaa au upungufu wa maji mwilini.

Hata hivyo serikali hawajatoa sababu zilizopelekea vifo hivyo vya watu hao ambao walikataa kutoka nje ya mgodi wakihofia kukamatwa na kufunguliwa mashtaka.

Polisi hata hivyo walisema wanaamini kuwa wamefanikiwa kuwaondoa watu wote waliosalia ndani ya mgodi na kuopoa miili yote baada ya mamia ya wachimba migodi kukwama kwa miezi kadhaa katika mgodi huo wenye kina kirefu wakifanya kazi kinyume cha sheria. **DW**

# CHIKOLA, SAADUNI VINARA MABAO MGUU WA KUSHOTO

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Tabora United, Offen Chikola na Nassor Saaduni wa Azam FC, wanaongoza kwa kufunga mabao kwa kutumia mguu wa kushoto katika Ligi Kuu Tanzania Bara, ambayo itarejea tena mapema mwezi ujao.

Kwa mujibu wa takwimu iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi, wachezaji wao wamefunga mabao manne kila mmoja hadi kumalizika kwa mechi za mzunguko wa kwanza.

Na kwa mujibu wa dawati ya takwimu la Nipashe, wachezaji hao wana mabao manne ya kufunga kila mmoja, hivyo hakuna bao hata moja kwa wachezaji hao walilofunga kwa mguu wa kulia wala kichwa, badala yale yake mabao yao wote wameyafunga kwa kutumia guu la kushoto.

Wachezaji wanaofuatia ni wale waliofunga mabao matatu kwa kutumia mguu huo ambao ni Hernest Malonga wa Coastal Union ambapo kwa sasa amerejea katika timu yake ,mama' ya Singida Black Stars, baada ya kuwachezea wagosi wa kaya kwa mkopo, Heritier Makambo na Tabora United, Gibril Sillah wa Azam FC, Joshua Ibrahim na Mishamo Daudi, wote wa KenGold.

Mgawanyo, kwa mujibu ya takwimu zetu unaonesha, Makambo ana mabao manne ya kufunga, moja akilifunga kwa mguu wa kulia, Mishamo na Joshua wa KenGold, wamefunga mabao matatu kila mmoja kwenye Ligi Kuu, hivyo yote wameyapachika kwa mguu wa kushoto.

Malonga na Sillah nao wamefunga mabao matatu kila mmoja katika ligi, na yote wametumia mguu huo.

Takwimu hizi zimetoka siku chache baada ya Bodi ya Ligi kumtangza kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua, kuongoza kupachika mabao kwa kutumia mguu wa kulia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo bado ipo mapumzikoni.

Ahoua, amepachika mabao saba kwenye Ligi Kuu mpaka sasa kwa kutumia mguu wa kulia.

Kiungo huyo raia wa Ivory Coast, amefunga mabao yote saba aliyonayo katika ligi kwa kutumia mguu huo.

Wanafuatiwa na mastraika wawili, Clement Mzize wa Yanga na Selemani Mwalimu wa Fountain Gate, wamefunga mabao matano kila mmoja kwa kutumia mguu huo.

Hata hivyo, wachezaji wote hao kila mmoja amefunga mabao sita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

# Ligi ya Wanawake kurejea kibabe

**Na Shufaa Lyimo**

RAUNDI ya 10 ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), inatarajiwa kuendelea tena kuanzia Jumanne kwa JKT Queens kuikaribisha Alliance Girls kutoka jijini, Mwanza kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Mechi nyingine ya ligi hiyo yenye timu 10 itazikutanisha Yanga Princess na Bunda Queens, mechi itakayochezwa kwenye Uwanja wa KMC, Mwenge huku Ceasiaa Queens itaumana na Fountain Princess huko mkoani Iringa.

Gets Program itamenyana na Mashujaa Queens kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma wakati Januari 22, mwaka huu Mlandizi Queens wataibakili Simba Queens kwenye Uwanja wa Kituo cha TFF kilichopo Kigamboni.

Mabingwa watetezi, Simba Queens yenye pointi 25 ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 20 lakini imecheza mechi moja pungufu, Mashujaa Queens yenye pointi 15 wao wanashika nafasi ya tatu.

Mlandizi Queens, mabingwa wa kwanza wa ligi hiyo kwa msimu wa mwaka 2016/2017 wao wanaburuza mkia wakiwa na pointi moja mkononi.

Bingwa wa ligi hiyo ataiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yanayofanyika kila mwaka kwa kushirikisha mabingwa wa nchi 12 wanachama wa shirikisho hilo.




Wachezaji wa Pamba Jiji FC ya jijini, Mwanza wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuchezwa kuanzia mapema Februari. **PICHA: MTANDAO**

# CAF yazitaka Simba Queens, Yanga GIFT

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI fainali ya kwanza ya Mashindano ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 ya Afrika (CAF U-17) maarufu GIFT inatarajiwa kufanyika kesho, Simba Queens na Yanga Princess, zimetakiwa kuanzisha timu za vijana ili kuongeza ushiriki wa klabu katika michuano hiyo mwakani.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Idara ya Maendeleo Soka la Wanawake wa CAF, Meskerem Tadesse, alisema wanahitaji kuona klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania na nchi nyingine kuanzisha timu za vijana ili kusaidia kuhasamisha na kutambua vipaji mapema.

Meskerem alisema uamuzi huo utasaidia kuleta maendeleo lakini pia utawapa nafasi wachezaji wasichana kujifunza mbinu sahihi za mpira wa miguu katika umri mdogo.

„Tunawahimiza wote wanaomiliki timu kuanzisha timu za wasichana wa umri chini ya miaka 17, tunatamani kuona mwakani idadi ya timu zitakazoshiriki mashindano haya zimeongezeka, najua timu kongwe za Tanzania hapa hazipo, mwakani tuzione,“ alisema Meskerem.

Aliongeza amefurahi kuona wachezaji wapya wametambuliwa lakini viwango vya timu vikiongezeka kutoka mechi moja kwenda nyingine.

„Hata kama timu inafungwa, lakini kuna kitu kinaonekana, juhudi, kujituma na kiu ya kutaka kufanya jambo zuri, huu ni mwanzo, tunaamini tutakuwa na mashindano mazuri zaidi wakati ujao,“ aliongeza kiongozi huyo.

JKT Queens na TDS Girls zote za Tanzania zitakutana kesho katika fainali ya michuano hiyo itakayochezwa kuanzia saa 12:00 jioni kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Klabu hizo mwenyeji zitakutana katika fainali hiyo baada ya kila moja kupata ushindi kwenye mechi za hatua ya makundi na hivyo kuongoza katika hatua hiyo ya awali.

Michuano ya mwaka huu kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati imeshirikisha timu saba, mbali na wenyeji wengine ni Kenya Sports Academy, Kenya Junior Athlets kutoka Kenya, City Light (Sudan Kusini), Aigle Nor ( Burundi) na Boni Consilli ya Uganda.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WAARABU KUMNG'OA SALAH

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 32, anatazamiwa kupewa ofa ya pauni milioni 65 ili kumshawishi kuondoka Liverpool na kuelekea Saudi Arabia msimu wa joto. (***Sun***)

### MADRID KUMFUATA TRENT

REAL Madrid wameachana na harakati zao za kuwania saini ya mlinzi wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, mwenye umri wa miaka 26, na watarejea kumchukua mlinzi huyo wa England msimu wa joto. (***Relevo***)

### GYOKERES, MBEUMO SOKONI

ARSENAL inafikiria chaguo la kuimarisha safu yao ya ushambuliaji huku straika wa Sporting na Sweden, Viktor Gyokeres, mwenye umri wa miaka 26, na mshambuliaji wa Brentford na Cameroon, Bryan Mbeumo (25), wakiwa kwenye orodha yao. (***L'Equipe***)

### RASHFORD KUTUA NAPOLI

NAPOLI ipo tayari kujiunga na kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England na Manchester United, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 27. (***Sun***)

### GARNACHO ANUKIA ITALIA

NAPOLI pia wana uhakika wa kumsajili, Alejandro Garnacho, mwenye umri wa miaka 20, kutoka Manchester United na wampempa winga huyo wa Argentina mkataba wa miaka mitano. (***Il Mattino***)

### ADARABIOYO KITAELEWEKA

KLABU ya Brighton imeonyesha nia ya kumnunua mlinzi wa kati wa England, Tosin Adarabioyo, mwenye umri wa miaka 27, ambaye alijiunga na Chelsea Julai, mwaka jana. (***Mail***)

### HARNANDEZ ATAJWA EPL

KLABU ya Deportivo La Coruna imekataa ofa kutoka kwa Chelsea kwa ajili ya winga wa Timu ya Taifa ya Hispania, Yeremay Hernandez, mwenye umri wa miaka 22. (Metro)

### WEST YAMUUZA GUILHERME

WEST Ham inataka kupunguza hasara kwa Mbrazil Luis Guilherme mwenye umri wa miaka 18, na kumuuza mshambuliaji huyo miezi saba tu baada ya kumsajili. (Times)

### UNITED YAMNADI ANTONY

MANCHESTER United imefanya mazungumzo na klabu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Real Betis, wakati wakijaribu kumtoa winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24 katika dirisha dogo la usajili la mwezi huu. (Sun)

### CHELSEA YAMKATAA GUEHI

CHELSEA haina uwezekano wa kumsajili beki wa England, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Crystal Palace mwezi huu baada ya kumrejesha Trevoh Chalobah (25), kutoka kule Selhurst Park alikokuwa akicheza kwa mkopo. (Mail)

### NEWCASTLE: KELLY HAUZWI

KLABU ya Newcastle United imekataa dau la pauni milioni 11 kutoka Fenerbahce kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa England, Lloyd Kelly, mwenye umri wa miaka 26. (Mail)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# NEYMAR AWINDWA NA TIMU TATU MAREKANI

**RIYADH,** Saudi Arabia

●●● Nyota huyo hakuwa na msimu mzuri na Al Hilal kutokana...

NYOTA wa Brazil na mshambulizi wa Al Hilal, Neymar yuko katika mazungumzo ya awali na timu tatu za Ligi Kuu Marekani (MLS), ikiwamo Chicago Fire FC, kuhusu uwezekano wa kuhama, kwa mujibu wa ESPN.

ESPN imeripoti kwa sasa Inter Miami sio miongoni mwa timu zinazomtaka Neymar, na kocha wake mpya, Javier Mascherano, amesema „haiwezekani" kumwongeza Mbrazil huyo kutokana na ukomo wa mishahara uliowekwa na MLS.

**Neymar mwenye umri wa miaka 32, amevumilia kipindi kigumu akiwa na Al Hilal tangu ajiunge na klabu hiyo ya Saudi Arabia kutoka Paris Saint-Germain msimu wa joto wa 2023 kwa ada ya dola milioni 97.6.**

Alipata majeraha ya misuli katika goti lake la kushoto alipokuwa kwenye majukumu ya kimataifa muda mfupi baada ya kujiunga na Al Hilal.

Neymar alirejea uwanjani Oktoba, mwaka jana lakini jeraha la misuli ya paja lililofuata limemzuia kutoa mchango zaidi msimu huu.

Kwa ujumla, amecheza mechi saba pekee za ligi na alifunga bao moja, katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa ya Asia dhidi ya Nassaji Mazandaran, Oktoba 3, mwaka 2023.

Hata bila Neymar, Al Hilal iliishinda Ligi Kuu ya Saudia msimu uliopita.

Mkataba wa nyota huyo wa zamani wa Barcelona unaendelea hadi Juni, mwaka huu na inamaanisha anaweza kuanza mazungumzo na timu nyingine kuhusu mkataba mpya.

Neymar anabakia kuwa mmoja wa watu wenye majina makubwa katika mchezo huo kutokana na uchezaji wake pamoja na Messi na Suarez wakati akiwa na Barca kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.

Wakati akiwa na klabu hiyo ya Katalunya alikuwa sehemu ya kikosi kilichoshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji mawili ya LaLiga na matatu ya Copa del Reys.

Baadaye alihamia PSG mwaka 2017 na kushinda mataji matano ya Ligue 1, mataji matatu ya Ufaransa na mawili ya Ligi.

Neymar alianza soka lake la kulipwa akiwa na Santos mwaka wa 2009, na kuwaongoza kwa ushindi wa Copa Libertadores (Ligi ya mabingwa Amerika Kusini) mwaka wa 2011 ambapo alifunga katika mkondo wa pili wa fainali katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Peñarol.

Katika ngazi ya kimataifa, Neymar ameichezea Brazil mara 128, akifunga mabao 79.

Alikuwa sehemu ya Brazil iliyoshinda medali ya dhahabu kwenye Michezo ya Olimpiki ya majira ya joto ya mwaka 2016, ambayo Brazil ilikuwa mwenyeji.

## HABARI MICHEZO

# RICE: TULISTAHILI KUFUNGA MABAO 10




**LONDON,** England

KIUNGO wa Arsenal, Declan Rice, amesifu uchezaji wa wachezaji wenzake katika mchezo wa dabi ya London dhidi ya Tottenham Hotspur, akisema walistahili kufunga mabao 10 katika ushindi wa magoli 2-1.

Kikosi cha Mikel Arteta kilitoka nyuma na kuwashinda Spurs katika pambano la burudani lililofanyika kwenye Uwanja wa Emirates, huku mabao yote matatu yakipatikana katika kipindi cha kwanza ambacho kiliwafanya wageni wachukue bao la kuongoza kabla ya Dominic Solanke kujifunga na Leandro Trossard akafunga la ushindi.

Arsenal walipoteza nafasi nyingi katika kipindi cha pili ili kuendeleza uongozi wao, na akizungumza na TNT Sports baada ya mchezo, Rice alisema walikuwa na nafasi ya kufunga mabao zaidi kwenye mchezo huo.


„Tuna bahati mbaya hatukufunga mabao 10, hiyo ndiyo hisia," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

„Hatuhitaji ujumbe, kucheza Spurs, kama huwezi kuinuka kwa hilo basi hupaswi kucheza soka. Tungeweza kuwa na mabao matano au sita.

„Usiku wa leo (juzi) ulikuwa na maana zaidi ya kitu chochote. Kuanzia dakika ya kwanza."

Arsenal sasa wako pointi nne nyuma ya vinara wa Liverpool, ambao wana mchezo mmoja mkononi.

# Garnacho njiapanda United



**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amesisitiza, Alejandro Garnacho, ana mustakabali katika klabu ya Manchester United huku akiendelea kuimarika katika mfumo wa kocha huyo licha ya kutakiwa Napoli.

Timu hiyo ya Serie A inatazamiwa kupata fedha za kutumia Januari mara Khvicha Kvaratskhelia atakapokamilisha uhamisho wake wa kwenda Paris Saint-Germain.

Vyanzo vimeiambia ESPN, Garnacho yuko kwenye orodha ya wachezaji wanaoweza kuuzwa, wakati matatizo ya kifedha ya United yanamaanisha wanaweza kuzingatia ombi lolote kubwa.

Lakini alipoulizwa kama Garnacho ana mustakabali chini yake pale Old Trafford, Amorim alisema: „Hilo liko wazi. Ana kipaji. Anatafuta njia bora ya kucheza kwenye mfumo huu.

"Anaimarika wakati wa mazoezi. Alianza mchezo wa mwisho. Hebu tuone."

Amorim alimtoa Garnacho katika kikosi chake kwa ushindi dhidi ya Manchester City hapo Desemba, mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alianza kwa mara ya kwanza kwa zaidi ya mwezi mmoja katika mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Arsenal siku ya Jumapili na Amorim anasema bado anaendelea kukubaliana na mahitaji ya mfumo mpya.

„Anahitaji kujifunza kucheza katika nafasi tofauti," alisema Amorim.

„Anahitaji kucheza vizuri zaidi ndani. Anaimarika sana katika nafasi ya kupona wakati hana mpira. Lakini kwa kufanya hivyo, wakati mwingine hayuko mahali sahihi kufanya mabadiliko kama alivyokuwa zamani."

# Ancelotti aanika siri usajili Madrid

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, alikutana na Mkurugenzi Mtendaji wa klabu hiyo, Jose Angel Sanchez, ili kujadili hali ya timu na chaguzi za usajili baada ya kupoteza kwa mabao 5-2 kwenye mechi ya Supercopa ya Hispania dhidi ya Barcelona iliyochezwa wikendi iliyopita.

Kwa mujibu wa ESPN kikao hicho kilikuwa cha kawaida na kilipunguza mzozo wowote na pande zote mbili zilijadili matatizo ambayo yameikumba hapo Los Blancos tangu kuanza kwa msimu huu.

Ancelotti na wasaidizi wake wameomba kuiongeza kwa wachezaji kwenye safu ya ulinzi katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi.

Madrid walikuwa karibu kumsajili Leny Yoro ili kugharamia kuondoka kwa Nacho lakini mchezaji huyo mchanga wa Ufaransa hatimaye alisaini Manchester United.

Alphonso Davies pia alilengwa lakini Madrid walitaka kuheshimu Bayern Munich na, licha ya majaribio katika mwaka huo, hawakujaribu kumsajili wakati alikuwa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake.

Madrid bado wanafuatilia mustakabali wa raia huyo wa Canada, lakini ripoti za hivi karibuni kutoka Ujerumani zinasema mchezaji huyo anaweza kuongeza mkataba wake na wababe hao wa Ujerumani.

Kama ilivyoripotiwa na ESPN, Madrid wanaendelea kutafuta mchezaji wa kuchukua nafasi ya beki wa kulia ambaye ni majeruhi, Dani Carvajal na Trent Alexander-Arnold wa Liverpool ndiye chaguo lao.

Hata hivyo, vyanzo vya ESPN vimesema Liverpool tayari wamekataa ofa kutoka kwa Real Madrid ya kutaka kumsajili beki huyo wa pembeni katika dirisha la uhamisho la Januari hii, hivyo kuna uwezekano kwamba wababe hao wa Hispania watasubiri hadi msimu wa joto kumsajili kwa uhamisho wa bure.



## Yanga ina njaa ya ushindi

INATOKA UKURASA 24

MC Alger, ina pointi nane kwenye nafasi ya pili, ikihitaji sare ya aina yoyote ili kufuzu kwani ikifanikiwa itakuwa imefikisha pointi tisa, Yanga itaambulia pointi nane.

Wakati huo huo, klabu hiyo imetangaza kumsajili winga mpya, Ikangalombo kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DR Congo).

Klabu hiyo imemtangaza Mkongomani huyo muda mfupi kabla ya dirisha dogo la usajili halijafungwa.

Ikangalombo anakuwa mchezaji wa pili kutambulishwa na mabingwa hao watetezi baada ya beki wa pembeni, Israel Mwenda, aliyetua Jangwani akitokea Singida Black Stars.

## Simba SC : Mpanzu alifunga usajili wetu

INATOKA UKURASA 24

ubora wao.

Tumekariri lazima dirisha la usajili likifika lazima timu isajili, au mmetuzoea kila dirisha ni lazima tusajili kwa sababu hatukuwa na timu bora na ya ushindani kwa miaka kadhaa nyuma, ndiyo maana kila dirisha ilikuwa ni lazima kuingia sokoni kusaka wachezaji kwa ajili ya kuboresha timu yetu, nadhani mazoea ndiyo yanawatesa watu hivi sasa na kushangaa kuona mpaka sasa hatujasajili.

Hii inatokana na ubora wa timu tuliobayo hivi sasa, tuna kikosi cha wachezaji ambao wanajitosheleza kabisa, ndiyo maana viongozi wetu na benchi letu la ufundi hawakuona sababu yoyote ya kusajili mchezaji mwingine katika kipindi hiki zaidi ya Elie Mpanzu pekee," Ahmed alisema.

Hata hivyo alisema Mpanzu walimsajili muda mrefu na muda ulipofika walikamilisha taratibu za uhamisho, hivyo kwao wanaona ni kama kipindi hiki hakuna mchezaji waliyemsajili.

"Huyu tulimsajili kwa muda mrefu, sema tu dirisha kubwa lilikuwa limefungwa, ndiyo maana tumekuja kumwingiza katika dirisha hili dogo, kwa maana hiyo safari hii hatujaona umuhimu wa kufanya usajili mpya kwa sababu ya ubora wa kikosi tuliochokuwa nacho.

Tungekuwa na uhitaji tungeweza kumsajili mchezaji yoyote yule ndani na nje ya nchi, lakini tuna wachezaji wazuri sana safari hii," alitamba Ahmed.

Alisema kikosi walichonacho kwa sasa japo kina wachezaji wengi wenye umri mdogo na si wazoefu, lakini kwa muda mfupi wamewapa matokeo chanya, lakini wakiwa na faida ya kufundishika na kuendelea kukua.

"Ni kikosi kinachoweza kutupa mafanikio makubwa, pia tunaweza kukikuza kwa sababu kina wachezaji vijana wanaoweza kuendelea kufundishika, ikumbukwe pia mafanikio haya ya kuongoza ligi na kufuzu robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika yasiwasahaulishe, bado tunatengeneza timu, tuko katika mchakato huo na unaonekana kwenda vizuri," aliongeza meneja huyo.

Alisema pia kikosi chao kinaendelea vyema na mazoezi kwa ajili ya mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Sfaxien itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

# LIGI KUU BARA KUANZA NA VIPORO VYA SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Nchini (TPLB), imesema Ligi Kuu Tanzania Bara itaanza kwa mechi za 'viporo' za Simba na Yanga, kabla ya kuendelea na raundi ya 17, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji mKuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema, ligi hiyo itarejea kuanzia mapema Februari kwa mechi kati ya Tabora United dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi na Yanga kuikaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

"Tumeshapokea taarifa rasmi CHAN haitakuwepo tena, ilikuwa ianze Februari Mosi hadi 28, lakini Kamati ya Utendaji ya CAF imepeleka mbele, tarehe maalum hawajataja, kwetu tumeipokea.

Tulisimamisha ligi kwa ajili ya Kombe la Mapinduzi pamoja na CHAN, Kombe la Mapinduzi limeisha na CHAN imepelekwa mbele, tafsiri yake ni lazima ligi irejee mapema. Mpango wa awali wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi ni kuanza tena mwezi wa pili," alisema Kasongo.

Aliongeza wakati ligi inasimama timu nyingi zilikuwa zimecheza michezo 16, kasoro timu nne (Simba, Yanga, Tabora United na Kagera Sugar), ambazo ndizo zilikuwa zimecheza michezo 15, hivyo kwanza ni lazima viporo hivyo vichezwe.

"Tuna viporo kwa klabu mbili kwa timu zilizokuwa zinashiriki Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, Simba na Yanga, ukitazama msimamo kuna timu zimecheza mechi 16, zenyewe zina michezo 15, nafikiri na Kagera Sugar pamoja na Tabora United, tafsiri yake tutaanza kwanza kucheza mechi hizo za viporo, ndipo ligi iendelee kwa michezo ya raundi ya 17," Kasongo alisisitiza.

Hata hivyo, alikumbushia klabu hizo pia hazijacheza mechi zao kwa Kombe la FA, hivyo kabla ya kucheza viporo vya ligi wanapaswa kwanza kukamilisha viporo vya michuano hiyo.

"Nadhani wataanza na Kombe la FA, na baada ya hapo watacheza michezo ya ligi, muda upo, kuanzia sasa mpaka mwanzoni mwa mwezi wa pili kuna kiasi cha wiki tatu, timu zitakuwa zimeshakusanyana kuanza mazoezi," aliongeza ofisa huyo.

Simba yenye pointi 40 ndio vinara wa ligi hiyo huku KenGold ya jijini, Mbeya inaburuza mkia katika msimamo ikiwa na pointi sita kibindoni.



Beki wa Azam FC, Landry Zouzou, akimiliki mpira katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na lala salama ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara itakayorejea tena kuanzia mapema mwezi ujao. **PICHA: MTANDAO**

# Azam FC yaifuata Mtibwa Manungu

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Azam FC kinatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani mkoani, Morogoro.

Kwa sasa Mtibwa Sugar yenye pointi 35 ndio vinara wa Ligi ya Championship ikifuatiwa na Mbeya City yenye pointi 34 kibindoni, lakini imecheza mechi moja zaidi ya timu hiyo inayowania tiketi ya kurejea tena katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, alisema mechi hiyo imeandaliwa ili kukiweka sawa kikosi chao kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ibwe alisema kikosi chao kinaendelea vyema na mazoezi na kila mchezaji yuko tayari kuipambania timu hiyo ili kufikia malengo waliyoyaweka.

Hata hivyo Azam FC ilitolewa mapema katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na vigogo wa Ligi Kuu ya Rwanda, APR na sasa inapambana kuhakikisha inamaliza katika nafasi ya juu ili kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa hapo mwakani.

Wakati huo huo, uongozi wa Azam umempa mkataba mpya beki wao wa kati, Landry Zouzou ambao utamalizika ifikapo mwaka 2028.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam yenye pointi 36 iko katika nafasi ya tatu nyuma ya vinara Simba yenye pointi 40 na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 39, hata hivyo imecheza mechi nmoja zaidi ya vigogo hao wa soka nchini.

# Michezo

Nipashe Ijumaa Januari 17, 2025




## Garnacho njiapanda United

UKURASA 22



Kibu Denis, Straika wa Simba

## Simba SC : Mpanzu alifunga usajili wetu

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba imeweka wazi sababu za kutofanya usajili wa mchezaji mpya katika kipindi cha dirisha dogo kilichofungwa juzi zaidi ya winga, Elie Mpanzu, ni kutokana na kuwa na kikosi bora na kilichokamilika.

Kabla ya msimu huu kuanza, Simba ilisajili wachezaji 17, ikiwa ni idadi kubwa ya wachezaji kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita, pia iliacha mastaa wake kadhaa kwa sababu mbalimbali ikiwamo kushuka viwango.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili jana baada ya vikao kati ya viongozi na benchi la ufundi, hawakuona sababu ya kuongeza mchezaji mwingine, hivyo kikosi kilichopo kitaendelea kucheza mechi za Kombe la Shirikisho Afrika, Ligi Kuu na michuano ya Kombe la FA.

Ahmed alisema hayo kufuatia klabu hiyo kukaa wakati timu mbalimbali zikiwa katika pilikapilika kuimarisha vikosi vyao huku zikihakikisha zinakamilisha mchakato huo kabla ya dirisha la usajili halijafungwa.

"Ukiona watu wanasajili kipindi hiki cha dirisha dogo ambacho hakuna wachezaji bora sana walio sokoni ujue walikuwa na mapungufu, ndiyo maana wamesajili, siyo suala ya kujivunia sana hasa kipindi hiki cha dirisha dogo, inabidi tu tujivunie viongozi wetu na benchi letu la ufundi kuwa dirisha kubwa tulilitumia vizuri sana kunasa wachezaji ambao mpaka sasa wapo katika

INAENDELEA UKURASA 23

# YANGA INA NJAA YA USHINDI

## Ramovic aifananisha mechi hiyo na 'kupanda mlima', Ikangalombo rasmi...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI imemtambulisha rasmi winga mpya, Jonathan Ikangalombo, Yanga imesema itaongeza umakini na haitarudia makosa ya kukubali kupoteza mechi kwenye uwanja wa nyumbani kama ilivyotokea walipokutana na USM Algers ya Algeria mwaka juzi, imeelezwa.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara waliruhusu kichapo cha mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na ushindi wa bao 1-0 ugenini haukuwasaidia kubeba taji la michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka juzi.

Yanga inatarajia kuwakaribisha MC Alger ya Algeria katika mechi ya mwisho ya Kundi A ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ushindi wa aina yoyote utaipeleka Yanga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo wakati MC Alger inahitaji sare ili kusonga mbele katika mashindano hayo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kwa sababu wanahitaji matokeo ya ushindi tu katika mchezo huo, viongozi na benchi la ufundi linaipa umuhimu wa kipekee mechi hiyo huku wakiongeza umakini tofauti na wanachama na mashabiki wanavyofahamu.



Kamwe alisema Yanga inawaonya wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuondoa dhana kuwa mechi hiyo itakuwa rahisi kwa sababu wanakwenda kucheza dhidi ya timu ngumu na iliyoshikiliwa hatima yao.

„Kuna tabia nimeiona kwa Wanayanga siku hizi. Yaani tunazungumza kama vile hii mechi ni rahisi sana, au MC Alger ni timu nyepesi na hii mechi imeisha, tunakosea sana, ni mechi kubwa na inahitaji maandalizi ya kutosha. Katika mchezo wa fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya ‚ndugu' yake huyu USM Alger, tulikuwa na mategemeo kama haya, tulidhani tutamfunga hapa na kwenda kupata sare ugenini, kule kujiamini kupita kiasi kulituponza na Waarabu watakatuadhibu. Wao wana faida hata sare inawabeba, naomba tuungane na kupeana sapoti kwa ajili ya kushinda mechi hii," alisema Kamwe.

Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, alisema maandalizi yanaendelea vyema huku akiwataka wachezaji wake waingie uwanjani kama hawajawahi kufanya kitu katika michezo yote iliyopita.

"Tuna mlima katika mchezo wa mwisho, kwetu ni kama fainali, najua utakuwa mgumu lakini nina imani kwa namna wachezaji wangu wanavyoonekana wana njaa ya kusaka ushindi.

Tunatakiwa kuingia uwanjani tukijiona kama vile hatujafanya kitu, tunatakiwa kuongeza umakini katika mchezo huu wa mwisho," alisema Ramovic.

Kocha huyo alitoa siri ya kuwakataza wachezaji wake kushangilia kupita kiasi katika ilivyokuwa katika mechi iliyopita waliyocheza dhidi ya Al Hilal Omdurman ambayo walipata ushindi wa bao 1-0.

"Niliwazuia wachezaji wangu kushangilia kupitiliza mara baada ya mchezo dhidi ya Al Hilal Omdurman ili akili ya kila mmoja aielekeze kwenye mchezo huu, nimefurahi kwa namna wachezaji walivyojituma kwenye michezo mitatu mfululizo waliyocheza, miwili dhidi ya TP Mazembe na mmoja uliopita," kocha huyo alisema.

Yanga, iko nafasi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi saba, ambapo inahitaji ushindi pekee ili kufuzu, ambapo itafikisha pointi 10 na kuiacha MC Alger ikisalia na pointi nane.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >